# DHANA YA MAISHA KATIKA NOVELA MBILI ZA EUPHRASE KEZILAHABI: *NAGONA* na *MZINGILE*

Na

**CHARLES IRUNGU MUNGAH**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA "MASTER OF ARTS" KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

University of NAIROBI Library
0472592 5

**JULAI, 1999**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

---------------------------------------------------
CHARLES I. MUNGAH
(mtahiniwa)

**Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii ya Chuo Kikuu**

---------------------------------------------------
Dkt. Mwenda Mbatiah

---------------------------------------------------
Dkt. Kithaka wa Mberia

## YALIYOMO


UNGAMO ---------------------------------------------------------------- i

YALIYOMO ---------------------------------------------------------------- ii

TABARUKU ---------------------------------------------------------------- iii

SHUKURANI ---------------------------------------------------------------- iv

MUHTASARI ---------------------------------------------------------------- vii

**1.0 SURA YA KWANZA---------------------------------------------------- 1**

1:1 TATIZO LINALOFANYIWA UTAFITI ---------------------------- 1

1:2 NADHARIA TETE ---------------------------------------------------- 2

1:3 MADHUMUNI YA TASNIFU -------------------------------------- 2

1:4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII ------------------------------ 3

1:5 MIPAKA YA TASNIFU ---------------------------------------------- 5

1:6 YALIOANDIKWA KUHUSU MADA HII ------------------------------ 6

1:7 MSINGI WA KINADHARIA -------------------------------------- 9

1:8 NJIA ZA UTAFITI ---------------------------------------------- 11

TANBIHI ---------------------------------------------------------------- 13

**2:0SURA YA PILI ---------------------------------------------------- 14**

2:1 UTANGULIZI---------------------------------------------------- 14

2:2 MAISHA YA MWANADAMU NA JUHUDI ZAKE -------------- 15

2:3 KUSHINDWA KWA JUHUDI ZA MASHUJAA-------- ---------26

2:4 KUSHINDWA KWA ASASI ZA MWANADAMU------------------29

2:5 ELIMU YA MWANADAMU NA MIPAKA YAKE----------------39

2:6 HITIMISHO---------------------------------------------------- 42

TANBIHI---------------------------------------------------------- 45

**3:0SURA YA TATU---------------------------------------------------- 46**

3:1 UTANGULIZI---------------------------------------------------- 46

3:2 MAANA YA MAISHA ---------------------------------------------- 48

3:3 KUKOSA FURAHA KWA MAISHA YA MWANADAMU -------63

3:4 DHANA YA UKWELI---------------------------------------------- 72

3:5 HITIMISHO---------------------------------------------------- 78

TANBIHI---------------------------------------------------------- 80

**4:0 SURA YA NNE---------------------------------------------------- 81**

4:1 UTANGULIZI---------------------------------------------------- 81

4:2 KUATHIRIWA KWA MWANDISHI NA MAZINGIRA MBALIMBALI UDHANAISHI-------------------------------------- 82

4:3 ATHARI NYINGINEZO---------------------------------------- 92

4:4 HITIMISHO ---------------------------------------------------- 100

TANBIHI---------------------------------------------------------- 102

**5:0 SURA YA TANO---------------------------------------------------- 103**

HITIMISHO

5:1 MUHTASARI WA MASUALA MUHIMU ------------------------ 103

5:2 MAPENDEKEZO---------------------------------------------------- 107

Kwa marehemu baba yangu na mama yangu mzazi aliyenisomesha na kunifanya niwe na ari ya kutia ghera na kufaulu masomoni.

# SHUKRANI

Kazi hii imeweza kutimilika bila ila kutokana na ukarimu na hisani ya watu mbalimbali. Ingawaje siwezi kuwataja wote kwa ukarimu na fadhila zao, ningependa kuwataja baadhi yao kwa wema na uadilifu wao. Mawazo na ushauri wao uliiwezesha kazi hii kufikia kiwango ilichofikia.

Awali kabisa nakishukuru Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunidhamini katika masomo yangu ya uzamili. Hali isingekuwa rahisi kwangu isingelikuwa ufadhili huu.

Nawatolea shukrani zisizo kifani wasimamizi wangu Dkt. Mwenda Mbatiah na Dkt. Kithaka wa Mberia kwa kuniongoza tangu mwanzo hadi tamati ya tasnifu hii. Uwanagenzi wangu haukuwakera bali uliwatia moyo wa kuniongoza kupitia njia za kweli na za kiusomi.

Aidha nawanyoshea mkono wa ahsante wahadhiri wengine wa Kiswahili kwenye Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika. Hasa ningependa kuwataja Dkt Kineene wa Mutiso, Margaret Njuguna, John Hamu Habwe, Basilio Mungania na James N. Michira. Misaada mbalimbali walionipa iliniopoa kutoka hali ya uhitaji. Vitabu walivyoniazima vilikuwa mbolea ya hekima.

Namkabidhi shukrani za udhati wa moyo Peris Mburu ambaye alinitia moyo wakati safari ilikaribia kuwa ngumu Yeye pamoja na Bi Kibinda nawashukuru kwa msaada wao pamoja na ushauri wao ambao uliniondolea hali ya fadhaa. Aidha natoa shukrani zangu kwa msaada walionipa wakati nikitayarisha tasnifu hii

Sina budi kutoa shukrani za kipekee kwa Timothy Arege ambaye alinitangulia mwaka mmoja katika Chuo Kikuu. Alinishika mkono pale ambapo sikufaulu. Waaidha namtunukia shukrani zangu kwa msaada wa vitabu na makala alizoniazima Singependa kuwasahau wanafunzi wenzangu Dominic Gicheru na Esther Mukewa kwa moyo wa ushirikiano ambao walidhihirisha kuwa nao Ukarimu na ushirika wao uliniondelea ukiwa na upweke

Ningependa kuwashukuru wafuatao kwa hisani zao na misaada yao ainati: dada yangu Ruth Mungah, Andrew Njung'e, Samuel Kahuha, John Kariuki na Isaac Mbira.

Hatimaye namshukuru Esther Mukina kwa kuichapa kazi hii kwa ustadi Aidha, nampa shukrani za kipekee Dickson Omungu kwa ukarimu wake na kwa kunipa nafasi kuihariri kazi hii katika kopyuta.

Daima nitabaki katika deni la wema wao kwani hakuna chochote ambacho chaweza kufidia ukarimu wao Hata hivyo, wote niliowataja na ambao sikuwataja nawatolea shukrani zisizo kifani kwani kwa njia moja au nyingine waliiwezesha kazi hii kutimilika

# MUHTASARI


Tasnifu hii imechunguza suala la maisha kati ya maudhui mengine katika novela mbili za kezilahabi *Nagona* na *Mzingile*. Tasnifu hii ina sura tano.

Katika sura ya kwanza tumebainisha tatizo la utafiti. Aidha tumebainisha madhumuni ya tasnifu, sababu za kuchagua mada hii pamoja na mipaka ya kazi hii. Waaidha tumefanya udurusu wa yalioandikwa kuhusu mada hii. Nadharia ambayo tumetumia ni ya kisosholojia ambayo baadhi ya kanuni zake ni kusaili mazingira kazi ya kifasihi ilimoibuka na mazingira alimoandikia msanii.

Sura ya pili imeonyesha juhudi mbalimbali za binadamu maishani katika kujaribu kuelezea ukweli na uhalisi wa maisha yake. Juhudi za mashujaa vilevile na asasi mbalimbali zimejadiliwa. Elimu ya mwanadamu na mipaka yake katika kuelezea maana ya maisha imezungumziwa.

Sura ya tatu imeyajadili masuala ya maana ya maisha na ikiwa kweli furaha inaweza kupatikana maishani mwa binadamu. Hatimaye sura hii imechunguza na kujadili dhana ya ukweli kama ambavyo msanii huyu amelisawiri suala hili katika *Nagona* na *Mzingile*.

Katika sura ya nne tumeonyesha vile ambavyo mwandishi ameathiriwa na mazingira alimoandikia na kuyamithilisha na mazingira ya kipindi ambacho udhanaishi uliweza kupata mwamko mpya huko Magharibi Aidha tumebainisha kuwa maisha ya msanii huyu na athari alizopata kutoka kwa waandishi na watetezi wa udhanaishi yameathiri mtazamo wake wa maisha vikubwa.

Hatimaye katika sura ya tano tumehitimisha kwa kutoa maoni yetu kwa ujumla kuhusu kazi hizi pamoja na masuala muhimu ambavo tumeyajadili katika sura za mwanzo Aidha tumependekeza kazi hizi zifanyiwe uhakiki zaidi hasa kwa upande wa fani

# 1:0 SURA YA KWANZA

## 1:1 Tatizo linalofanyiwa utafiti

Katika kazi hii tumezihakiki novela mbili za Euphr Kezilahabi kwa kuangalia maana ya maisha. Tunatarajia kuchunguza mtazamo wa mwandishi huyu wa maisha huku tukitathmini falsafa yake kuhusu suala la maisha. Maswali tutakayokuwa tukijiuliza ni:

> Kulingana na mwandishi ni nini maana ya maisha?[1] Maisha ni kitu gani?

Kazi ambazo tumezihakiki ni novela za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991). Tumechagua novela hizi mbili kutokana na sababu kwamba suala la maisha limewahi kuandikiwa katika riwaya zake zingine, ambazo ni *Rosa Mistika* (1971), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1981), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Kichwamaji* (1974), na wahakiki mbalimbali. Wahakiki hao ni kama vile: P.M. Masau (1985), Senkoro (1982), B.T. Wambui (1992) n.k.

Aidha katika *Nagona* na *Mzingile* mwandishi, amelipa suala la maisha mtazamo tofauti na riwaya za hapo awali. Maudhui yameongelewa kwa mtazamo tofauti na riwaya za hapo awali. Maudhui yameongelewa kwa mtazamo wa kifalsafa kuliko katika riwaya zake zingine za hapo awali.

## 1:2 Nadharia tete

Katika tasnifu hii haipothesia ambazo tutakuwa tukitahini ni :

a) Maisha ya mwanadamu hayana furaha

b) Maisha ya mwanadamu hufuata mkondo fulani ambao mwenyewe hana uwezo nao

c) Mwanadamu hujitahidi kuyaondoa maisha yake kwenye mkondo wake.

## 1:3 Madhumuni ya tasnifu

Awali kabisa ni kuchunguza maana ya maisha kulingana na E Kezilahabi Hapa tutaonyesha mtazamo wa mwandishi kuhusu suala la maisha na sababu za maisha ya binadamu kuwa na mkondo fulani

Pili, tutazisaili sababu za mwandishi kuwa na msimamo alionao kuhusu maisha Hapa tutaonyesha jinsı mazingira mbalimbali ya jamii yake yalivyoathiri mtazamo na uandishi wake Haya ni mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo huathiri mtu ye yote yule aliye katika jamii yo yote ile Aidha elimu yake imeathiri vipi uandishi wake. Mtu haandiki katika ombwe tupu Mwandishi yeyote yule huandika mambo ambayo

huyaona yakitendeka kila siku na mambo haya hutokana na tajriba yake katika jamii inayohusika Hii ndio sababu kuu ya nadharia ya kisosholojia kutilia maanani hoja ya kuchunguza mazingira kazi ya kifasihi ilikoibuka Vilevile tutatizama kuathiriwa kwa mwandishi na waandishi wengine hasa wenye kutetea udhanaishi

Tatu, tutaliangalia suala la maisha kama kichocheo cha mwandishi kuandika kazi hizi mbili tunazozishughulikia

## 1:4 Sababu za kuchagua mada hii

Tumeichagua mada hii kutokana na sababu kwamba hili ni suala muhimu katika maandishi na kazi nyingi za mwandishi huyu na takriban limejitokeza katika kazi zake zote

Tumechagua kuzihakiki novela za E Kezilahabi kutokana na umashuhuri wake katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili Mchango wake si haba katika kuendeleza fasihi ya Kiswahili Mbali na riwaya na mashairi aliyotunga, ameandika katika majarida[2] mbalimbali juu ya fasihi ya Kiswahili na uchambuzi wa vitabu vya fasihi na amewahi kushiriki katika makongamano mbalimbali ya kimataifa ya fasihi ya Kiswahili

Kazi za Kezilahabi za hapo awali zimeshughulikiwa na wahakiki wengi katika viwango mbalimbali. Hata hivyo tunanuia kulipa suala la maisha uzito unaofaa kwa jinsi ambavyo halikupewa hapo awali hasa katika novela hizi mbili. Tutatumia nadharia na mtazamo tofauti na ule uliyowahi kutumika katika kuchambua kazi hizi.

Aidha msimamo wa E. Kezilahabi kuhusu maana ya maisha ya binadamu umejitokeza kwa uwazi zaidi katika kazi zake za hivi karibuni – *Nagona* na *Mzingile*. Hapa Mwandishi amelipa suala la maisha mtazamo tofauti na riwaya za hapo awali. Ameliongelea suala hili kwa njia ya usanii na kifalsafa jambo ambalo limedhihirisha kupevuka kwake kimawazo na kisanaa. M.M. Mulokozi (1983:1) amedai hivi kuhusu mwandishi huyu katika riwaya yake ya *Rosa Mistika:*

> Mwandishi si mpevu katika uzoevu wa maisha. maisha anayoyajua ni yale ya kijijini kwao na yale ya kishule migogoro na matatizo ya vijana wa shule – hasa ya kimapenzi – yanachukua sehemu kubwa ya riwaya hiyo.

Lakini tunapomchunguza mwandishi huyu katika novela hizi mbili tunamwona akimulikia suala la maisha kwa njia angavu na ya kifalsafa. Mafumbo na jazanda ainati zimetumika tangu mwanzo hadi mwisho.

Masuala ambayo mwandishi huyu ameyaongelea katika novela hizi mbili ni masuala ambayo hayatokei tu katika jamii yake, bali katika jamii nzima ya ulimwengu Katika kazi hizi mbili mwandishi ameliangalia suala la maana ya maisha na ukweli kati ya maudhui mengine Haya ni masuala ambayo binadamu amekuwa na maswali mengi juu yake, kwa muda mrefu, bila kuwa na majibu timilifu. Vilevile tunatarajia tahakiki yetu itatupia mwangaza novela hizi mbili na kuhimiza tahakiki za aina hii ili kuendeleza fasihi ya Kiswahili

## 1:5 Mipaka ya tasnifu

Kama ambavyo tumetaja awali, tunanuia kujikita katika kazi mbili za E Kezilahabi na ambazo tumekwishazitaja

Mbali na kazi hizi mbili, mwandishi huyu vilevile ameandika riwaya ambazo ni : *Rosa Mistika* (1971) *Kichwamaji* (1974), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1981). Diwani alizotunga ni *Kichomi* (1974) na *Karibu Ndani* (1988) Vilevile mchezo wa kuigiza na hadithi fupi

Hatutazihakiki kazi hizi zote kutokana na upana na muda mfupi uliopo wa kuandika tasnifu hii. Hata hivyo, novela zake mbili *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) zitatudhihirishia jinsi ambavyo mwandishi analitazama suala la maisha Hii haina maana kwamba tutazipuuza hizo kazi zingine, la Tutakuwa tukizinukuu pale ambapo itakapofaa

## 1:6 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii

Kazi za E Kezilahabi zimefanyiwa tahakiki na wahakiki wengi katika mada mbalimbali Hata hivyo suala la maisha kama alionavyo mwandishi halikupewa uzito kama ambavyo tunadhamiria kulipa katika utafiti wetu na hasa katika novela mbili tunazozihakiki Wahakiki mbalimbali wameandika juu ya dhana na maana ya maisha katika kazi nyinginezo za mwandishi huyu Tahakiki hizi zitatufaa ili kuelewa falsafa ya mwandishi kuhusu maisha na kutufunulia maana yake kama anavyolijadili swala hili katika novela hizi mbili Hata hivyo, hakuna tahakiki ambayo imeshughulikia maana ya maisha katika novela hizi mbili ambazo tunazishughulikia

Senkoro (1982) katika kitabu chake *Fasihi* amechambua maudhui mbalimbali yanayopatikana katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na

kuelezea falsafa ya E. Kezilahabi kuhusu maisha kwa muhtasari tu. Kazi hii itatufaa ili kuelewa zaidi mwelekeo wa mwandishi.

P.M. Musau (1985) katika tasnifu yake ya M.A, ambamo alishughulikia riwaya za *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1981), amegusia suala la maana ya maisha. Hata hivyo Musau amefanya hivyo katika kutaka kuonyesha mwandishi (E. Kezilahabi) kama mtu aliyekata tamaa. Anatetea dai hili kwa kuonyesha dunia kama uwanja wa fujo na mahala pasipo na furaha. Ingawa suala la maana ya maisha limepewa nafasi ndogo kazi hiyo itatufaa ili kutuonyesha msingi wa mwandishi katika suala la maisha.

B.T. Wambui (1992) amezihakiki riwaya za *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1981) na *Gamba la Nyoka* (1979). Anataja kwa kupitia *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) anapomwangalia Kezilahabi kifalsafa. Ingawaje hazami kwenye novela hizi kwa undani huku akionyesha mazingira alimoandikia mwandishi ili kuelewa msingi wa falsafa na msimamo wake mwandishi, sehemu ambayo ameandika juu ya falsafa ya mwandishi itatufaa.

M.M. Mulokozi amechambua *Dunia Uwanja wa Fujo* na kubainisha maudhui yanayojitokeza kama ndoa, uchawi, siasa, uhusiano kati ya mtu

binafsi na jamii na maisha kuwa 'fujo'. Ameyataja vilevile masuala makuu yanayopatikana katika riwaya zingine pamoja na mashairi ya Kezilahabi. Ingawa falsafa ya Kezilahabi kuhusu maisha imepewa nafasi ndogo, kazi hiyo itatufaa kwani itatupa mwangaza zaidi kuhusu mwandishi huyu na falsafa yake.

Mhakiki yeyote yule hunufaika na kuwa mwangavu zaidi kwa kusoma kazi mbalimbali za wahakiki ainati ili kuweza kuitathmini kazi yake. Ni kwa sababu hii basi tumezisoma tahakiki za wahakiki mbalimbali kama vile M. Msokile, M. Mbatiah, K. Wamitila, L.A. Mbughuni, mwandishi mwenyewe E. Kezilahabi n.k. Mtazamo wao wa mada tunayoandikia utatufaa si haba.

Kwa muktadha huu basi ni wazi kuwa novela mbili ambazo tumezihakiki hazijapewa nafasi kubwa ya uhakiki kama tunavyodhamiria kufanya kwa kuzingatia msimamo wa mwandishi kuhusu maisha na maana yake. Aidha mada hii imejiweka bayana zaidi katika novela hizi mbili kuliko katika kazi zake zingine za hapo awali.

## 1:7 Msingi wa kinadharia

Nadharia mahususi kama mwongozo wa kuhakiki kazi fulani ya fasihi ni muhimu kwani huwa kama dira ya kumwongoza mhakiki.

Nadharia tutakayoitumia kuzihakiki kazi hizi za E. Kezilahabi ni ile ya kisosholojia (Sociological). Nadharia hii imetumika sana hivi karibuni hasa na wahakiki wanaotoka kwenye jamii zenye historia ya ukoloni chambilecho Eddah Gachukia (1983:33).

Mtu anayesifika kama mmoja wa waasisi wa nadharia hii ni Hippolyte Taine (1828 - 93). Aliiangalia kazi ya kifasihi kama picha ya kijiografia, kimazingira na kitamaduni ambamo kazi hiyo imezuka. Kwamba kazi ya fasihi inaweza kuchukuliwa kama rekodi ya kweli ya maisha ya watu.

Alidai kuwa, riwaya kwa mfano, ni kioo mwafaka cha kuonyeshea vipengele vyote vya maisha ya jamii. Alisisitiza kuwa fasihi kwa ujumla haiwezi kutengwa na harakati za mwanadamu, ambazo zinaongoza maisha yake. Hiki ni kipengele muhimu katika nadharia hii na tunadhamiria kukitumia katika kuzihakiki kazi mbili tulizozichagua. Kipengele hiki huhusisha fasihi na jamii na maisha ya jamii kwa ujumla. Hili ndilo suala analosisitiza Ngugi wa Thiong'o (1977:xv) anaposema:

> Fasihi ni dhihirisho la ujumi na ubanifu wa jamii katika kupigana na mazingira yake ili kuweza kupata mahitaji ya maisha, chakula, mavazi, makazi na katika mfanyiko huo kuumba na kujiumba upya katika historia. (Tafsiri yetu).

Ili kuonyesha kuwa fasihi ni zao la jamii naye Robert Escarpit (1971:3) anasema:

> Bila msingi wa kijamii, ukweli wa fasihi hubatilishwa sawa na wa ramani isiyo na vitu vya kimaumbile
> (Tafsiri yetu)

Kipengele kingine muhimu cha nadharia hii na ambacho tutakitumia ni kile ambacho husisitiza kwamba mhakiki hawezi kuhakiki kazi ya fasihi bila kuzingatia mazingira yake - mazingira na maisha ya mwandishi. Siyo kazi yake tu inayochunguzwa bali pia vipengele vilivyo nje ya kazi - hii ni kumaanisha maisha ya kijamii yaliyozaa kazi yake. Mazingira hayo ni kama yale ya kisiasa, kiuchumi n.k. Nadharia hii inapinga mitazamo ya nadharia ambazo hutazama fasihi kama asasi ambayo imejisimamia. Nadharia ya uhakiki mpya, kwa mfano, husisitiza kuwa mtaala wa fasihi

unapasa kuanzia na kuishia katika nyanja ya fasihi, isihusu jamii wala mwandishi aliyetunga.

Nadhari hii hufuata utaratibu kama ule wa sayansi Kama vile watafiti wa somo la Biolojia (Biology) wanavyotilia maanani mazingira wanamoishi viumbe ndivyo wahakiki wa fasihi nao wanapasa kuzingatia mazingira ya kazi ya fasihi wanayoihakiki Hizi ni sifa za kazi za kifasihi kwa kuzihusisha kazi hizo na mazingira zinamotoka

Kwa mkabala huu tutajitahidi kuchunguza mazingira alimoandikia mwandishi. Mazingira haya yatakuwa ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Aidha maisha ya mwandishi, elimu yake na jinsi ambavyo haya yote yameathiri uandishi na utunzi wake

## 1:8 Njia za utafiti

Tumeifanya kazi hii haswa kupitia utafiti wa maktabani Tutazisoma novela mbili tunazozishughulikia kikamilifu pamoja na kazi zake zingine na vilevile makala mbalimbali ambayo mwandishi huyu amekwisha andika Jambo hili litatuwezesha kumwelewa zaidi msanii huyu

Ili kuitekeleza dhamira yetu kikamilifu tutazipitia kazi zote za hapo awali zinazoshughulikia uhakiki wa vitabu vinginevyo vya E. Kezilahabi na hasa zenye kugusia mada tutakayoijadili. Aidha kazi yoyote ya kifasihi hasa inayogusia maudhui tunayoshughulikia na vitabu vya taaluma nyingine vyenye kujadili mada ya maisha vitatufaa. Tutasoma kikamilifu makala na maandishi yanayohusu nadharia tutakayoitumia.

Mazingira anamoishi mwandishi, uhusiano wake na jamii, tamaa yake, juhudi, mafanikio na kutofanikiwa kwake huathiri mawazo na mtazamo wake kuhusu maisha. Ili kuelewa vizuri kazi ya mwandishi fulani na kufahamu ni nini kichocheo cha kazi yake, ni bora kumfahamu mwandishi mwenyewe. Ni kwa sababu hii tutajitahidi kupata historia ya msanii huyu. Basi tutasoma makala yoyote yenye kusimulia historia yake na ya Tanzania ya wakati huo.

Ili kufaulisha kazi hii, tutazungumza na kupata mawaidha kutoka kwa wataalamu wa fasihi.

## TANBIHI

[1] Kamusi ya Kiswahili sanifu imeeleza maisha kama:
a)kitambo cha kiumbe kuwa hai
b)namna ya kuishi.

[2] Majarida kama vile Kiswahili na Mulika

# 2:0 SURA YA PILI

## 2:1 Utangulizi

Katika sura hii tutazichunguza juhudi mbalimbali za binadamu katika kujaribu kusaka ukweli unaodhihirishwa na maisha yake. Binadamu huwa katika bidii kubwa ya kuelezea ukweli huu. Juhudi zake mbalimbali ndio hujumlisha maisha yake. Hata hivyo juhudi hizi hazifikii mbali kwani huwa hana uwezo.

Aidha tutatalii juhudi za mashujaa mbalimbali na watu ambao walifikiriwa kuwa wameshikilia ukweli. Tutajadili mchango wao katika kujaribu kutatua kitendawili cha maisha.

Asasi mbalimbali za binadamu huwa vilevile mbioni zikijaribu kumtatulia binadamu fumbo la maisha yake. Katika sura hii tutachunguza mchango wa asasi za dini na selikali katika kumtegulia binadamu kitendawili cha maisha yake.

Hatimaye tutachunguza elimu ya binadamu na umbali ambao imemfikisha. Tutachunguza mchango wa elimu hii katika maisha ya binadamu kwa jumla na mahala pake katika kusaka maana ya maisha na ukweli unaodhihirishwa nayo.

## 2:2 Maisha ya Mwanadamu na Juhudi Zake

Katika novela za *Nagona* na *Mzingile*, mwandishi ametusawiria maisha ya mwanadamu kama ambayo yamezingirwa na juhudi zake mbalimbali za kutafuta ukweli na uhalisi wa maisha Tunaonyeshwa hii kama safari ya mwanadamu na katika safari hii anakuwa kama anazunguka kwenye duara Mwandishi anatumia sitiari ya sayari na jua kuonyesha jinsi maisha ya binadamu yalivyo (*Mzingile* uk.5). Sayari huwa mbioni kulizunguka jua. Vivyo hivyo binadamu huwa mbioni kuusaka ukweli na uhalisi wa maisha yake na ni kana kwamba huwa mbioni kulizunguka jua lake lisiloonekana

Hizi ni juhudi za binadamu katika kutafuta uhalisi wa maisha na kuishi maisha ambayo hayana vilinge. Lakini katika juhudi zake hizi, binadamu hujikuta akizunguka mahala pale pale pamoja Maisha ya binadamu yanafananishwa na jinsi sayari zinavyozunguka jua. Kulingana na sayansi ya unajimu sayari huwa katika mwendo wa kuzunguka jua.Kila sayari hufuata mkondo wake, mfano wa duara, na huchukua nyakati mbalimbali kutegemea umbali wake kutoka kwa jua. Kuna vilevile mwendo mwingine ambao ni kuviringika kwa sayari, hususan dunia, katika mhimili (axis) ambao huishikilia. Ni mwendo huu wa pili ambao husababisha usiku na mchana.

Mwendo huu huwa ni ule ule wa kujirudia. Kezilahabi anamithilisha maisha ya binadamu na mwendo huu wa kuzunguka mahali pale pale akiwa mbioni kuusaka ukweli na uhalisi wa maisha yake ambao haupatikani. Jua ndilo hutoa miale ili dunia iweze kupata mwanga. Katika novela zote mbili sitiari ya mwanga imetumika kuwakilisha ukweli. Lakini katika juhudi zake za kutafuta ukweli huu , mwandishi amemsawiri binadamu akizunguka mahali pale pale kama sayari zifanyavyo. Katika *Nagona*(uk.24) babu anasema kuwa ni mara chache sana alikaribia nagona, ambayyo ni sitiari mwandishi ametumia kurejelea ukweli. Kila alipoukaribia ulirudi kinyumenyume naye alizidi kuufuata. Binadamu huwa mbioni kujaribu kuutafuta ukweli katika maisha yake. Hata hivyo katika papara zake binadamu huwa hana uwezo bali huongozwa na nguvu fulani.

Ukweli huu umegumbikwa na maluweluwe na binadamu hauoni tena. Mwandishi anaelekea kudai kuwa maisha ya binadamu ni wazi kama yalivyo wala kutafuta ukweli ambao haupatikani ni bure tu. Maisha yake ni wazi kama yalivyo lakini amekuwa kama kichaa kwa kutafuta kilichowekwa wazi.

Haya ni maisha ya mwanadamu ambayo yeye hujaribu kuyatolea majibu masuala magumu yayahusuyo. Huu ni ukweli ambao anausaka lakini

hataupata. Mwandishi ameupa sifa mbali mbali. Mara nyingi binadamu atajidai amekaribia kuupata ukweli lakini kama asemavyo, hatapata nafasi ya kuuweka mikononi mwake. Ni kana kwamba jinsi anavyotia ghera ya kufikia ukweli huu ndivyo unavyozidi kumtoroka.

Jambo moja msanii huyu amesisitiza hapa ni kufikiri. Ni katika kufikiri tu ndipo binadamu atakaribia ukweli. Kuweza kupata ukweli kunahitaji juhudi kubwa kwani hata wale ambao walipata kuuweka mikononi mwao uliwaponyoka hatimaye. Ukweli huu basi una sifa za kutodhibitika na umezingirwa na maluweluwe na basi inakuwa muhali kuweza kuufikia.

Kezilahabi anayaona maisha kama ambayo binadamu hana haja ya kujishughulisha nayo bali kuyaishi kama yalivyo. Maisha yake ndiyo anapaswa kuyazingatia lakini yeye hujishughulisha kutafuta ukweli ambao haupo na basi anasema , "Hatuoni tena kilichowekwa wazi." (*Nagona* uk.44)

Hoja ya mwanadamu kutokuwa na uwezo wa kupata ukweli kuhusu maisha yake na kwamba juhudi zake huishia tu kumzungusha kwenye duara ile ile imejiweka bayana zaidi katika diwani ya mwandishi huyu ya *Kichomi*(1974:13) kupitia taswira ya ng'ombe aliyefungiwa mtini anasema:

Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka

Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa,

kila mpigo wa moyo wangu

Huu mpigo muziki wa maisha. (uk.13)

Historia ya mwanadamu ina watu maarufu waliowahi kuishi na kufanya juhudi kubwa katika kujaribu kuelezea maisha ya binadamu. Wanafalsafa wengi wamewahi kulijadili suala la maisha ya binadamu kwa kirefu lakini yote hayo ni bure bilashi, kwani hayakumpa binadamu jibu la ukweli ausakao. Ndiyo sababu kizee kinasema hivi katika *Nagona:*

> Mashujaa wote wamezikwa katika kilima hiki, hapa! Lile pale mlionalo kama pango, yasemekana ni kaburi la Yesu. Lile pale lenye udongo mwingi ni la Muhammad. Hapo mlipokanyaga ni kaburi la Marx, na lile pale ni la Socrates. (uk. 19)

Kwa kufungamana na nadharia ya kisosholojia tumeongelea baadhi ya wanafalsafa hawa na athari zao kwa Kezilahabi katika sura ya IV. Marx na Socrates walikuwa wanafalsafa mashuhuri ambao mwegemeo wao uliathiri , na bado unaathiri viongozi na wasanii wengi.

Katika sakasaka zake za maisha na ukweli unaodhihirishwa na ulimwengu, mwanadamu alibuni kiumbe chenye nguvu kuliko zake na kisichoonekana Walikiita kiumbe hiki Mungu na huu ukawa mwanzo wa mwanadamu kuabudu Shida zilipomfika alizielekeza kwa Mungu Walianza kumtolea kafara na sadaka Katika novela ya *Mzingile*(uk.4) tunaambiwa kuwa watu walipofikwa na janga la moto walifanya jitihada kubwa kumwelezea Kakulu[1] kama mtu mnene kinyume na walivyomfikiria na kumwona akiwa mtu mfupi na mwenye machachari. Walianza kutoa sadaka chini ya mbuyu ili kumtambikia.

Baadaye mwanadamu alimhusisha Mungu katika kila jambo alilotenda na shida zilipomfika alizishtakia kwa Mungu. Mungu hapa anatazamwa na mwanadamu kama shuluhisho la shida zinazomkabili na hasa katika kuelezea kitendawili cha maisha yake. Katika novela ya *Mzingile* msimulizi amesema hivi:

> Lakini bila wewe hakuna tena kitakachoshikilia na kuweka kwa pamoja fikra zetu (uk.32)

> Nilikuwa nimesafiri mwendo kiasi. Moyoni nilikuwa nikijiuliza kama kulikuwa na uwezekano wa kutoka nje ya duara ya mzee[2] (uk 43)

Kama ambavyo tumekwisha tangulia kusema baada ya binadamu kutia juhudi kubwa kujaribu kusaka ukweli unaodhihirishwa na maisha yake, analemewa na kukimbilia katika imani katika Mungu Binadamu anajiona kama ambaye hana uwezo na nguvu zozote bila Mungu Hata fikra zake zitakoma kufanya kazi kwani kama asemavyo - hakuna tena kitakachoshikilia

Baadaye inakuwa ni vigumu hata kufarakana na mawazo ya imani katika Mungu, kama asemavyo mwandishi Imani hii vilevile inakuwa kama duara Binadamu hujiendeshea mambo yake lakini hukimbilia Mungu wakati yupo kwenye shida . Mawazo haya inakuwa kana kwamba ni duara ambayo Mungu amemwekea binadamu.

Binadamu anaitisha uhuru kutoka kwa Mungu lakini Mungu anasema kuwa yeye ndiye anayehitaji uhuru kutoka kwa binadamu kwani binadamu anamfuata kila mahali Yaani inakuwa ni vigumu kwa binadamu kuishi bila Mungu. Binadamu anamtafuta Mungu kanisani, msikitini, makaburini, mbuyuni na hata ndani ya magofu kama mzee asemavyo (*Mzingile* uk 58).

Hata hivyo Mwandishi amekariri haja ya mwanadamu kufikiri Matatizo ya mwanadamu yatasuluhishwa na yeye mwenyewe wala sio imani

potovu. Kama nadharia ya kisosholojia inavyotilia mkazo, mazingira ambamo kazi ya kifasihi ilikoibuka ni muhimu katika kuhakiki kazi hiyo. Matatizo mengi na shida ambazo Kezilahabi amesawiri binadamu akikabiliana nazo zinatokana na mazingira fulani ambayo tutayajadili katika sura ya IV. Katika matatizo haya, kufikiri ndiko kutampeleka mbele binabamu. Katika novela ya *Nagona* hoja hii imekaririwa na kusisitizwa na mwandishi. Babu anamwambia msimulizi hivi:

> Usiwe na haraka. Kuna vikwazo vingi lakini kushinda vikwazo si kufikia kweli. Safari ni ndefu,lakini kusafiri si kufika. Jambo muhimu ni kufikiri (uk. 24)
> (msisitizo wetu)

Mwandishi hapa anasema kuna vikwazo vingi maishani katika kuusaka ukweli. Safari ya kuusaka ukweli ni ndefu na yenye pingamizi nyingi. Tumekwishaona jinsi njia imezongwa na miba na hata mashujaa hawakuimudu. Jambo ambalo mwandishi anatilia mkazo ni kufikiri ili kuweza kukabiliana na vikwazo hivi.

Mungu anakataa kusingiziwa kuwa yumo katika fikra za binadamu na anamwambia binadamu ajiamini (*Mzingile* uk.33). Kezilahabi anaona

imani katika Mungu kama ambayo inampotosha binadamu badala ya kujiamini yeye mwenyewe na kutumia muda wake mwingi katika kufikiri

Mwanadamu hana budi kutumia muda wake mwingi kufikiria njia za kujiondolea matatizo yanayomkabili. Ni katika kufikiria na kufanyia majaribio uvumbuzi wake ndio atakapokaribia suluhisho la shida zinazomkabili. Ni kwa sababu hii kijana aliyekuwa bondeni anasema kuwa kama binadamu angetumia muda wake mwingi katika kuwaza na kufanya majaribio angekuwa amepiga hatua kubwa kimaendeleo na kivumbuzi. Anauliza binadamu anashindwa nini kugundua mchanganyiko wa chembe hai? (*Mzingile* uk 50). Uvumbuzi na ushindi utatokana tu na binadamu kuendelea kufanya majaribio na kuwaza.

Mwandishi anampa moyo binadamu kwamba kama angetumia muda wake mwingi kuwaza na kufanya majaribio, hata kifo angekuwa amekishinda. Msanii huyu anaona kifo kama ambacho kimemshughulisha binadamu kwa kipindi kirefu, jambo ambalo halimsaidii. Anasema kuwa wazo la chanzo cha maisha yake na kifo vimempumbaza binadamu kwa muda wa karne nyingi wala havikusaidia katika kutatua kitendawili cha maisha yake. Mawazo haya yanakubaliana na ya Ignace Lepp (1968:139) ambaye anasema:

> Badala ya kufikiria kifo kama mwisho wa maisha, napendekeza tukitazame kama kitendo cha mwisho katika kutimiliza maisha ya muda. Basi itafuatia kwamba tukifaulu katika kuyapa maisha yetu maana, vivyo hivyo kifo kitakuwa na maana.(Tafsiri yetu)

Hoja ya kutojiketia na kushtakia Mungu imejidhihirisha katika riwaya ya Kezilahabi ya *Gamba la Nyoka* (1979:19) ambapo mwenyekiti wa kijiji cha Kisole anawaambia wanakijiji wenzake:

> Ndugu, wanakijiji. Wazee walisema, 'Mungu' anakulinda na wewe unajilinda. Kitendo ambacho tumekata shauri kutenda ni cha kishujaa lakini cha hatari. Tusitegemee tu kuwa Mungu yupo. Tujiandae...

Aidha mwandishi ametusawiria mwanadamu akiwa katika harakati za kujiimarisha kiviwanda. Juhudi zote za mwanadamu hulenga katika kuimarisha maisha yake. Mwandishi anauona ulimwengu kama uliojaa matatizo mengi ambayo husababisha maafa ya watu wengi. Anakariri haja ya kufikiri ili kuyatatua matatizo haya kupitia kwa msimulizi anayesema:

.. Kwa wakati huu serikali ilikuwa imetupa kazi ngumu ambayo tulihisi ingetufungulia njia mpya za kufikiri na kutatua matatizo ulimwenguni... Nchi nyingi katika ulimwengu wa tatu zilipata pigo kubwa...(*Nagona* uk 18). (msisitizo wetu)

Kezilahabi kama mwandishi ambaye ameshuhudia hali hii miongoni mwa jamii yake ya Tanzania ameichambua kwa upana zaidi. Mwandishi ameshuhudia hali ngumu ya kiuchumi ya nchi yake changa - hali ambayo hutawala nchi nyingi za ulimwengu wa tatu (suala hili tutalijadili kwa kirefu zaidi katika sura ya 4).

Siyo matatizo tu ya kiuchumi ambayo yanayasakama mataifa ya ulimwengu wa tatu bali pia njaa na kuzorota kwa viwanda hali ambazo huchangia matatizo ya ulimwengu. Kezilahabi kama mwandishi wa jamii iliyoko katika ulimwengu wa tatu ameathiriwa na mazingira haya, athari ambazo zimejitokeza katika kazi zake.

Mwandishi anauona ulimwengu kama mahala ambapo panafaa kuimarishwa ili paweza kumfaa mwanadamu. Ulimwengu wapaswa kutunzwa katika juhudi za mwanadamu za kujiendeleza. Basi anasema kupitia kwa kijana aliyekuwa bondeni akifanya majaribio katika maabara

kuwa hatupaswi kuutumia ulimwengu na kisha tuondoke badala yake twapaswa kuona kuwa wajibu wetu si kuutumia bali kuutunza(*Mzingile* uk.50).

Hii ni kutokana na sababu kuwa binadamu hutumia kila kitu kilicho karibu naye katika juhudi za kutaka kuyaimarisha maisha yake Kijana huyo anasema kuwa, "Mwili wa binadamu ni kiwanda kitegemeacho mali ghafi ya kila aina ulimwenguni." Hii ni kumaanisha kuwa binadamu hutumia chochote kile ambacho anaweza kukifikia kwa minajili yake bila kujali hali ya baadaye ya ulimwengu. Juhudi zote hizi huelekezwa katika hali ya binadamu kuimarisha maisha yake

Katika uhai wake basi, mwanadamu amefanya jitihada za kujiimarisha na kuvinjari ulimwengu unaomzunguka. Jitihada zake na harakati zake hujumlisha maisha yake. Fikra za mwanadamu ndizo dira yake itakayomwongoza. Ni katika fikra na kuwaza ambapo mwanadamu aligundua uwezo wake na akawa kiumbe cha ulinganisho, kukadiria na kupanga mambo yake kama Nietzsche[3] anavyodai. Friedrich Nietzsche (1844-1900) alikuwa mwanafalsafa mashuhuri wa maadili. Mtazamo wa mwandishi hata hivyo umeegemea zaidi falsafa ya udhanaishi, suala ambalo tumelijadili kwa kirefu katika sura ya IV.

## 2:3 Kushindwa kwa Juhudi za Mashujaa

Katika *Nagona* na *Mazingile* suala la kushindwa kwa asasi za mwanadamu kumpa majibu kuhusu ukweli na maana ya maisha limejiweka bayana. Juhudi za mwanadamu za kuimarisha maisha yake zimejidhihirisha katika asasi mbalimbali alizozibuni yeye. Lakini asasi hizi hazimpi jibu la suala analolisaka yeye. Hata watu mashuhuri na mashujaa waliotarajiwa kuwa karibu na ukweli hawatoi majibu. Ni sababu hii mwandishi akawalaza kwenye makaburi yalioachiwa kuharibiwa na wanyama na vichaa hujisaidia humo. Kizee kinaeleza:

> Mashujaa wote wamezikwa katika kilima hiki, hapa! Lile pale mlionalo kama pango, yasemekana ni kaburi la Yesu Lile pale lenye udongo mwingi ni la Muhammad Hapo mlipokanyaga ni kaburi la Marx,na lile pale ni la Socrates (*Ngona uk. 19)*

Mahala walipozikwa mashujaa hawa hapaheshimiwi tena kwani ng'ombe hawaishi kuyakwaruza makaburi hayo kwa kwato na kuyagongagonga kwa pembe. Na vichaa nao hujisaidia humo. Basi wamesalimu amri ya kifo na juhudi zao hazikufikia mbali. Binadamu naye amebaki kulemewa na kitendawili kile kile cha maisha. Watu mashuhuri na mashujaa

waliotarajiwa kuwa karibu na ukweli hawapo tena Njia walizodai kuonyesha na madaraja walioweka zinatiliwa shaka na binadamu kwani si kweli. Ngazi na vipandio walivyoweka haviaminiki kwani hata nao wamepigwa mweleka na maisha haya magumu.

Hawa ni watu mashuhuri waliowahi kuishi na kuheshimiwa na jamii ya ulimwengu. Yesu na Muhammad wametumika hapa kama viwakilishi vya dini ya Kikristo na ya Kiislamu. Yesu anashikiliwa na wakristo kama mkombozi wa ulimwengu[4]. Aidha makaburi ya viongozi wa nchi zenye uwezo mkubwa wa kiuchumi na kibiashara: Uingereza, Marekani, Ufaransa na Ureno yapo. Hawa ni wawakilishi wa viongozi wa kisiasa. Lakini wote sasa wamo makaburini wa kielekea kutokomea kwenye kaburi la sahau.

Mashujaa waliofikiriwa kutoa majibu kuhusu maisha ya mwanadamu hawakufanya hivyo. Ndiyo sababu mwandishi anawaonyesha wakiambiwa wasafishe roho zao. Mafunzo waliyotoa hayakumtatulia mwanadamu shida zake Muda katika novela hizi umepewa kipindi kirefu sana - mamilioni ya miaka - kumaanisha kuwa miaka nenda miaka rudi historia ya binadamu haijabadilika sana. Katika *Nagona (uk.15)* Msimulizi anafahamishwa kuwa wale ambao akonao walifika kule maelfu ya miaka iliopita Hao ni akina Plato, Socrates , Aristotle, Hegel, Darwin, Marx,

Freud na Niezsche. Hawa walikuwa wanafalsafa mashuhuri na ambao walifanya bidii katika kuelezea maisha na hulka ya binadamu

Mbali na bidii na ghera waliofanya katika kuyaeleza maisha na hulka ya binadamu suala muhimu la ukweli na uhalisi wa maisha ya binadamu halikujibiwa. Ni kwa sababu hii mwandishi amesema kuwa hiki ni kikundi kidogo tu cha waliokuwa wabishi katika usakaji wa njia. Walikuwa wabishi kwani kila mmoja wao alikuwa na mshikilio na tetezi ambazo zilipingana na ya wenziwe. Walitetea falsafa zao ambazo ziliwavutia wafuasi wengi baadaye. Aidha mwandishi ameendelea kusema kuwa hiki ni kikundi cha watu walioiwekea njia miba na daraja zisizo aminika. Hata hivyo, Kezilahabi ameathiriwa na baadhi ya kazi zao na suala hili tutalichunguza kwa kirefu zaidi hapa chini. Mafunzo na misimamo yao iliongezea kilinge katika kuyapa maisha maana. Walikuwa wakijaribu kupiga hatua kutoka kwa wale waliowatangulia lakini katika kufanya hivyo wakaongeza mizingo katika mzingile. Wameelezewa hivi katika *Nagona:*

> ...Ilibidi wafungwe vitambaa machoni kwa sababu walikuwa karibu kukata tamaa. Njia niliiweka wazi, tena wazi kabisa, wima bila kupinda, ukungu wote niliuondoa. Hiki ni Kikundi kidogo tu cha wale walioiwekea njia miba,

ngazi za kupandia na madaraja yasiyoaminika Walijaribu kuondoa miba, ngazi na madaraja yaliyowekwa na wale waliowatangulia, lakini kwa kufanya hivyo wakaweka vikwazo vingine badala yake . (uk.15)
(msisitizo wetu)

## 2:4 Kushindwa kwa asasi za mwanadamu

Awali kabisa tunashuhudia kushindwa kwa dini kama asasi Katika juhudi za mwanadamu za kusaka ukweli wa maisha na uhalisi wake, dini imekuwa ni asasi mojawapo muhimu. Masuala muhimu yahusuyo maisha na ambayo mwanadamu huwa hana majibu yake huelekezewa kwa Mungu kupitia dini. Lakini katika novela mbili za *Nagona* na *Mzingile* mwandishi amethibitisha kushindwa kwake katika kutoa jawabu toshelevu. Ndiyo sababu padiri anajibiwa ifuatavyo na Babu, anapowauliza wazee kama miongoni mwao hamna mkristo:

"Mbona unacheza ngoma yako nje ya duara ?"(*Nagona* uk.10)

Waumini huwa na njia zao za kusaka ukweli ilhali "wapagani", kama anavyowaita mwandishi, huwa na njia zao. Ndiyo sababu Babu anamwambia Padiri anacheza ngoma yake nje ya duara.

Kuhusu "mwana wa Mungu – Mkombozi", Babu anasema hivi:

> "Alipotea njia karne nyingi zilizopita. Ila nyayo aliziona... Atakuonyesha nyayo tu, kwa maana hata yeye hajapata kumshika...."(Ibid).

Dini imeshindwa kumpa jawabu analotaka mwanadamu na viongozi wake wameonyeshwa wakiwa walevi Msimulizi anapoingia nyumba moja alikoelekezwa na mama mwenye mimba anamkuta Padiri ambaye tunafahamishwa na mwandishi kuwa ni mlevi kupindukia (*Nagona* uk .4). hata siku ya Ngoma Kuu hakuweza kuhudhuria Hii ni siku ambayo makundi mbalimbali yalitarajiwa kutoa mwelekeo wa maisha Ilipofika jioni alikuwa chakari Ngoma zilipoanza, alijaribu kutembea lakini miguu yake haikumchukua Alikunywa mvinyo hadi akafa.

Viongozi wa dini walipaswa kuwa kielelezo cha kufuatwa na watu wengine hasa katika maisha na mienendo yao. Lakini kama ambavyo Kezilahabi ameyasawiri maisha katika novela hizi mbili - kitendawili kigumu - hata wale ambao walipaswa kuwa kielelezo chake wamelemewa na mtihani huu mgumu Badala yake wanajiingiza katika mambo ya ulimwengu na wanakuwa walevi kupindukia. Basi dini kama asasi

muhimu maishani mwa binadamu imelemewa kwa vile viongozi wake wameonyeshwa kama watu wasiofuata kanuni zake

Padiri mzungu naye alisali, akasali wee! wapi! Ukame haukwisha Katika kukata tamaa na alipoona watu wameanza kutoa makafara katika mibuyu, alianza kunywa sana pombe kali za kwao Zilipokwisha akanywa gongo Msimulizi anasema hivi kumhusu

> Katika ulevi wake alivunjavunja baadhi ya masanamu kanisani. Alisikika akipiga kelele. 'Mungu gani wewe! Umeniaibisha mbele ya watu weusi'[5] Alipoanza kuchanganya gongo na mvinyo, masista walimkimbia (*Mzingile* uk.20).

Siyo dini ya Kikristo tu iliyoshindwa bali ya Kiislamu vilevile. Ndiyo sababu mwandishi anatuonyesha makaburi walipozikwa Yesu na Muhammad – Muhammad akiwakilisha Uislamu Kifo kimewashinda (*Nagona* uk 19). Sheikh (mwakilishi wa dini ya Kiislamu) naye aliwachekesha watu Alipoona mambo yanazidi kuwa mabaya alijiolea visichana vidogo vitano, akidai pepo huanzia hapahapa ulimwenguni (*Mzingile* uk.20 ) Mwandishi anawaonyesha hawa viongozi wa kidini kama watu wa ulimwengu uliozingirwa na masuala yale yale magumu

kuhusu maisha. Sheikh anaamua kutokomea kwenye anasa kwani dini yake haimpi jibu.

Waaidha viongozi hawa wa kanisa wana hisia kama wanadamu wengine wa kawaida. Padiri anapandwa na hamaki na kumtusi msimulizi ambaye alienda kutubia kwake. Mwandishi anashauri tuanze misingi mipya (*Mzingile* uk 19)

Anaona imani ya dini kama kizuizi cha mwanadamu kufikiri. Na ni katika fikra tu ndiyo mwanadamu atakaribia ukweli na uhalisi wa maisha yake Kwenye riwaya yake ya *Gamba la Nyoka* (1979:19), kupitia mwenyekiti wa kijiji cha Kisole, Kezilahabi anasema:

> Ndugu wanakijiji wazee walisema 'Mungu' anakulinda na wewe unajilinda. Kitendo ambacho tumekata shauri kutenda ni cha kishujaa lakini cha hatari. Tusitegemee tu kuwa Mungu yupo. Tujiandae

Katika nukuu hii mwandishi anaelekea kupinga imani katika Mungu ambayo husababisha uzembe na hali ya kutojali. Imani katika Mungu haitamstawisha wala kumpa binadamu jibu la masuala yanayomkera Binadamu hapaswi kuketi tu na kutegemea kuwa Mungu yupo bali bidii

na kufikiri kutampeleka hatua mbele katika kutatua masuala yake. Msanii anaendelea kuibeza dini kwenye riwaya yake ya *Rosa Mistika* (1971 59) ambapo mhusika Rosa anasema

> "Wokovu maana yake nini? Wokovu! Wokovu gani! Kama kuna moto basi nitakwenda."

Serikali ni asasi nyingine ambayo mwandishi amebainisha kushindwa kwake. Serikali ni asasi muhimu katika maisha ya mwanadamu. Serikali huwa imetwikwa mzigo wa kuongoza, kulinda na kumpa mwanadamu mahitaji ya msingi. Tangu jadi historia ya mwanadamu imetawaliwa na kuwepo kwa viongozi wa kisiasa ambao huwa na wadhifa wa kuongoza serikali zao. Juhudi kubwa hufanywa na viongozi hawa ili kuimarisha chumi za nchi zao kwani ndiyo mizani ya kupimia utajiri na uwezo wa taifa fulani. Aidha nchi zenye uchumi imara na uwezo mkubwa wa kiuchumi huhakikisha kuwa maisha ya watu wake yamelindwa na takriban hutoa mahitaji yote ya msingi. Hata hivyo, mwanadamu huendelea kukabiliwa na swali gumu huku akijiuliza maisha ni nini? Ukweli na uhalisi wake ni upi?

Viongozi wa mataifa yenye uwezo mkubwa wa kisiasa na uchumi hutizamwa kama mashujaa na ambao watasuluhisha matatizo haya ya mwanadamu na ulimwengu kwa jumla. Kinyume na matarajio haya, Euphrase Kezilahabi ameonyesha kushindwa kwao katika majukumu haya. Hawa viongozi wa mataifa yenye uwezo mkubwa hawakutatua ukweli ni upi kwani bali na umashuhuri na sifa zao wamekufa na mahali walipozikwa hapaheshimiwi tena Kizee kinasema katika *Nagona* (uk 19) kuwa mahali walipozikwa wafalme wa mataifa mashuhuri ulimwenguni, kama vile Uingereza na Marekani, palikuwa mahala pa kuheshimiwa lakini sasa pameachiwa kuharibiwa.

Nchi hizi zinatambulika kwa uwezo wao mkubwa wa kiuchumi na kisiasa. Mataifa ya ulimwengu wa kwanza yanatazamwa na yale ya ulimwengu wa tatu kama kielelezo cha maisha ambayo yanastahiki. Viongozi wa nchi hizi hushikiliwa kwa heshima na huonekana na wengi kama kielelezo cha maisha ambayo yanastahiki. Lakini maisha ni kitendawili na kama ambavyo Kezilahabi amewasawiri viongozi hawa vilevile wameshindwa na kifo na makaburi yao yameachiwa kuharibiwa na muda usio mrefu watasahaulika. Msingi na njia ambazo walionyesha zinakuwa siyo jibu la kitendawili cha maisha, ambalo binadamu yumo kulisaka.

Siasa hujaribu kuwaweka wanadamu wote sawa Hasa kiini cha siasa za ujamaa ni kutekeleza usawa wa mwanadamu na kuondoa matabaka katika jamii. Hasa nadharia ya Marx hutetea dai kuwa amani itapatikana duniani tu iwapo jamii ya ulimwengu itaweza kuondoa matabaka ambayo yameitawala historia ya binadamu Hii ni katika bidii ya kuonyesha kuwa maisha ya mwanadamu yafaa yawe sawa Marx aliendelea kueleza kuwa mfumo wa usoshalisti ndio mfumo wa hali ya juu kabisa na ambao utakomesha vita vya kitabaka.

Katika *Mzingile (uk15)* tunaona vile ambavyo mazingira alimoandikia mwandishi yalimwathiri Nchi ya Tanzania iliamua kuzingatia siasa za usoshalisti katika azimio la Arusha la mwaka 1967 (suala hili tutalirejelea baadaye). Mwandishi aonekana kuubeza mfumo huu na anawaita wanasiasa walevi ambao wanaimba nyimbo za siasa (maongozi ya kisiasa) ambayo hawajui maana yake Mzee anauliza, "Nini hasa maana ya wimbo huo?"(uk. 15)

Mwandishi anawaita walevi kwani mengi ya mambo ambayo wanasiasa hawa husema huwa hayatekelezwi au hayawezi kutekelezeka. Hizi zote huwa ni juhudi za mwanadamu za kuelezea na kufasili maisha yake Katika mtazamo huu wa maisha Kezilahabi anaathiriwa na mazingira yake

kama mwanajamii wa Tanzania huru iliozingatia sera za mfumo wa usoshalisti. Mzee na msimulizi wanajibizana hivi

> "Ha! Yaani sifa yangu ya 'Mgawaji wa yote' pia imepotea!"
>
> "Wanasema watagawana wenyewe sawa kwa sawa na kuondoa matabaka."
>
> "Matabaka! Mbona mnatunga maneno ambayo hayamo katika kamusi yangu!" (uk.15).

Wanasiasa wanaonekana wakifanya bidii za kusawazisha tofauti zilizopo baina ya wanadamu. Lakini mwandishi anaelekea kupinga kauli hii kwani kama msimulizi asemavyo maisha ni kama mkufu unachukua kipande hiki na kile unaviunganisha. Kipande kimoja kikikataa unakiacha kisichofaa kwako kitamfaa mwingine (*Mzingile* uk 6). Wazo la kila mwanadamu kuyaendesha maisha yake limekaririwa vilevile katika riwaya ya Kezilahabi ya *Dunia uwanja wa Fujo* (1975:92) ambapo amesawiri Dunia kama uwanja wa fujo. Kwamba kila mwanadamu ameumbwa kufanya fujo zake halafu ajiondokee na kuna watu wengine ambao hufanya fujo zaidi ya wengine. Basi kwa maoni ya Kezilahabi dunia ni mahala pa kufanya fujo. Maisha ya binadamu ni fujo kwani

katika shughuli zake mbalimbali za kujiendeleza huwa hasa kama fujo sawa na vurumai iliyotokea wakati wa Ngoma Kuu (*Nagona* uk.59)

Serikali za mataifa mbalimbali zimo mbioni kuimarisha chumi zao na basi kuimarisha maisha ya watu. Lakini harakati zao zimeishia hata kutishia maisha yayo hayo. Nchi za ulimwengu wa tatu zimeonyeshwa zikiwa katika shida nyingi. Mwandishi ametoka nchi ya Tanzania na kama mataifa mengine ya ulimwengu wa tatu ina matatizo mengi ya kiuchumi na kisiasa. Nchi hizi zinakabiliwa na matatizo mengi ya kisasa na vita vya kikabila. Matatizo haya yote yameleta maafa mengi na kama ambavyo imeelezwa mamilioni ya watu walikufa (*Nagona* uk 19)

Serikali zimeonyeshwa zikiwa katika bidii kubwa ya kuboresha hali ambayo imeendelea kuzorota. Hali inazorota kutokana na kusambaratika kwa uchumi kwani viwanda vingi vimekufa na baadhi ya vile ambavyo vimesalia vinafanya kazi kwa hasara (*Nagona* uk 19). Basi serikali inatoa jukumu la kutalii mipaka ya kukagua na kuimarisha viwanda na uchumi kwa jumla. Hii yote ni ghera ya binadamu katika kuimarisha maisha yake.

Lakini mwandishi amedhihirisha kushindwa kwa asasi ya serikali katika azma hiyo. Juhudi na bidii za serikali zimeonyeshwa zikizunguka mahali pale pale kama afanyavyo binadamu kwani baada ya miaka kadhaa

wataalamu wengine walikuja kufanya utafiti ule ule Ni kana kwamba serikali nayo imewekewa duara na imo kuzunguka katika duara hivo bila kutoa suluhisho la matatizo ya wanachi wake Wataalamu baada ya wataalamu wanalipwa kufanya utafiti ule ule huku kukiwa na imani kwamba suluhisho la shida za binadamu litapatikana

Hii ni kumaanisha kuwa maisha yale ambayo yalitarajiwa kuimarishwa na binadamu ili kuishi vyema zaidi haiwezekani. Badala yake pesa zinaendelea kutumika katika miradi bubu Binadamu huzunguka duara katika jina la kutatua matatizo yake Kwani huwa hayaishi na hivyo basi kujikuta pale pale alipoanzia

Siasa na uongozi vinakuwa hata tishio kwa uhai wa mwanadamu Msimulizi aliporejea kutoka alikoenda kumwona mzee alikuta wanadamu wote wameangamia (*Mzingile* uk 53). Aliona haya yameandikwa kwenye sehemu moja nyeusi ya ukuta ambao ulikuwa umeanza kufifia

> Kwa watakaosalia Msifanye makosa tuliofanya sisi Tulifunzwa hatukufunzika Hatukuweza kuongoza mkondo wa sayansi na uchumi. siasa iliposhika hatamu Yote myaonayo ni kumbukumbu tu ya ujinga wetu

Mwandishi anaelekea kuunga mkono hoja ya kuangamia kwa binadamu kutokana na siasa

## 2:5 Elimu ya Mwanadamu na Mipaka yake

Katika kusaka ukweli na uhalisi wa maisha binadamu amezama katika elimu na falsafa kama ambavyo imejitokeza katika novela hizi mbili (*Nagona na Mzingile*) Hata hivyo, jitihada za binadamu kuelezea maana ya maisha kupitia elimu – sayansi na teknolojia – zinaonekana kuemewa Badala yake uwezo wake na elimu vinaishia kuwa tishio kubwa kwa uhai wake.

Mwandishi anasema kuwa viongozi wakuu wa dunia walikutana na muda mfupi baadaye ajali za mitambo ya nyuklia zikatokea (*Nagona uk. 23).* Viongozi wakuu wa dunia wanawakilisha mataifa yenye uwezo mkubwa kiviwanda na teknolojia. Teknolojia ya mataifa haya ni tisho kubwa kwa uhai wa binadamu kwani uhai wake umo katika hatari ya kuangamizwa na maendeleo haya. Awali tumeona kwamba mwandishi ametilia mkazo haja ya binadamu kujitatulia matatizo yake kwa kutumia motifu ya kufikiri Lakini kutokana na ajali za mitambo hii ya nyuklia wahusika wake wanajiuliza. " swali moja bado latusumbua je kufikiri

kungaliko?" (uk 23). Mwandishi anaelekea kuuliza je ikiwa binadamu atajiangamiza bado yuwafikiri?

Mwandishi anaona hatari ya jamii ya binadamu ikiangamia kutokana na hatari iliopo ya elimu yake. Maangamizi haya yanatokana na mabomu ya nyuklia ambayo ameyabuni yeye mwenyewe. Mabomu hayo yanatumika kama zana za vita. Yanasababisha maafa makubwa kwani watu wanakufa kama panya (*Mzingile* uk.45). Wanaosalia wanadhoofu, hata hawana nguvu ya kuchimba makaburi yenye kina cha kutosha. Kwa hivyo badala ya elimu ya binadamu kutumika katika kuimarisha na kutatua kitendawili cha maisha yake, inakuwa ni zana ya kummaliza na maisha yanakuwa hayana maana.

Binadamu anashindwa kuongoza mkondo wa uvumbuzi wake kwani hata bomu ambalo linasababisha maafa mengi linadondoshwa kwa bahati mbaya - ajali. Basi matukio muhimu maishani mwake yanasababishwa na ajali. Elimu ya binadamu inakuwa ya kukatisha tamaa.

Mwandishi ana wasiwasi na tabia ya binadamu kuelezea kila kitu kupitia sayansi. Binadamu amepumbazwa na sayansi na teknolojia na kuyafanya maendeleo haya mawili yaonekana kama kwamba ndiyo yanayoishi. Msimulizi anajibiwa hivi na kijana aliyekuwa akiishi bondeni

> Nina wasiwasi na falsafa yoyote inayojaribu kufanya sayansi na teknolojia vitawale kuwako kwa binadamu na mwishowe kuwa kitovu cha fikra. Sayansi na teknolojia havifikiri (*Mzingile* uk.45).

Sayansi na teknolojia vimetumiwa na binadamu kuharibu uasili wa maumbile huku akijaribu kutafuta ukweli unaoyaviringa maisha yake. Mfano ni mitambo ya kisayansi ambayo hurahisisha mambo (*Mzingile* uk14). Mwandishi anaona maendeleo na uvumbuzi wa mitambo hii kama wenye kuchangia vurumai za dunia kwani kama asemavyo inaleta mapinduzi mapya. Mabomu yanasababisha uharibifu mkubwa wa mali na maumbile - hii ndiyo mwandishi anaiita 'miundo yako' (ya Mungu).

Basi katika ghera ya binadamu anafaulu tu kuzusha vurumai huku akijiacha katika kilinge kile kile kinachogubika ukweli na uhalisi wa maisha.

## 2:6 Hitimisho

Juhudi mbalimbali za binadamu za kusaka ukweli na maana ya maisha yake zimejidhihirisha katika sura hii Binadamu amefanya bidii kubwa katika kujaribu kuyaelezea maisha yake mwenyewe Lakini ukweli ni kana kwamba umejificha mahali ambapo hapajidhihirishi. Mwandishi kama mwanajamii wa jamii pana ya ulimwengu amelijadili suala ambalo ni nyeti na la kutatanisha Hata hivyo, tumedhibitisha mwandishi ameathiriwa vikubwa katika mtazamo huu na mazingira yake (Sura ya IV imelijadili kwa kirefu zaidi suala hili). Nadharia ya kisosholojia hutilia mkazo hoja ya kusaili mazingira kazi ya fasihi ilimoibuka na maisha ya mwandishi Mazingira haya na maisha ya mwandishi huathiri mtazamo wake wa maisha . Kwenye dibaji ya diwani yake ya *Kichomi* (1974 XV) anasema hivi:

> . wazo moja hasa lilinisumbua. Jambo lenyewe lilikuwa swali linalohusu maana ya maisha. Swali hili liliukera sana moyo wangu
>
> (msisitizo wetu)

Mwandishi amekuwa akikerwa na suala la maisha kwa kipindi kirefu na amelijadili kwa mapana na marefu kupitia kazi zake mbili *Nagona* na

*Mzingile*. Katika kufanya hivyo mtazamo wake umeathiriwa na mambo kadha wa kadha ambayo tumeyataja

Katika sura hii vilevile tumejadili kulemewa kwa juhudi mbalimbali za binadamu kumpa jibu la swali hili nyeti. Watu mashuhuri na waasisi wa dini hawatoi jibu. Na kama mwandishi anavyosema baadhi yao waliwekea njia miba na daraja zisizovukika

Asasi zilizobuniwa na mwanadamu vilevile zimo katika bidii ya kutatua suala hili lakini ukweli umebaki kumkwepa na kumwepuka mwanadamu. Ndio sababu Padiri na Sheikh wanakufuru. Dini haiwapi suluhisho.

Serikali nayo imetia kani. Lakini imeishia kuvuruga na kusababisha maafa ya watu kutokana na siasa na vita. Hizi zote mwandishi anaziona kama ni vurumai ambazo ndizo hasa maisha.

Elimu ya binadamu imejadiliwa pia na ni katika bidii vilevile ya binadamu kujaribu kutatua utata wa maisha yake. Hata hivyo, elimu ya mwanadamu inatokea kuwa zana hatari ya kummaliza kupitia mitambo hatari ya nyuklia

Wazo moja ambalo mwandishi anaelekea kusisitiza ni haja ya binadamu kufikiri. Hoja hii imekaririwa hasa katika novela ya *Nagona.* Katika novela ya *Mazingile* hoja hii imekaririwa vilevile katika bidii ya binadamu kufanya majaribio mbalimbali ya viwanda.

Katika sura ifuatayo tutachunguza maana ya maisha kulingana na mwandishi huyu na falsafa yake kuhusu maisha. Kama anavyosema ukweli unapodhihiri uwongo hujitenga. Tutachunguza ukweli wa maisha na ikiwa maisha ya mwanadamu yana furaha kama ayaonavyo mwandishi.

**TANBIHI**

---

[1] Sitiari ya Mungu

[2] Mzee hapa anarejelewa kumaanisha Mungu

[3] Katika Ansell – Pearson, K (1960): Nietzsche contra Rousseau. University press Cambridge, uk14

[4] Tazama Biblia Takatifu Luka 2:11

[5] Kulingana na historia dini ya Kikristo ililetwa bara la Afrika na Wazungu.

# 3:0 SURA YA TATU

## 3:1 Utangulizi

Kezilahabi ameyasawiri maisha ya binadamu kama kitendawili kigumu katika *Nagona* na *Mzingile*. Jibu la kitendawili hiki halipatikani, naye binadamu basi yupo katika jitihada za kusaka jawabu hilo. Anafanya bidii kubwa ili kutatua ni nini maana ya maisha. Maisha ni fumbo kama ambavyo mwandishi ameliweka bayana suala hili katika *Nagona* na *Mzingile*.

Katika kulifafanua suala hili Kezilahabi ameonyesha falsafa yake kuhusu maisha. Kama nadharia ya kisosholojia inavyosisitiza mwandishi huandika kutokana na tajriba yake kati ya wanajamii anamoishi. Alivyofanya Kezilahabi ni kuliweka suala la maisha bayana kama ambavyo analishuhudia katika jamii pana ya ulimwengu. Hata hivyo, mwandishi huyu ameathiriwa kwa kiasi kikubwa na waandishi wenye kushikilia mtazamo wa udhanaishi (Existentialism) pamoja na mazingira alimoandikia. Mtazamo wa aina hii umeitwa 'utamaushi',[1] 'uhuria'[2] na 'majaaliwa'[3] na wahakiki wengine. Suala hili tutalijadili kwa kirefu katika sura inayofuata.

Amelifafanua suala la maisha ya binadamu na kuonyesha uwezo na mipaka yake. Ni mtazamo huu ambao umewapelekea wahakiki wengi wa kazi zake kufikia kauli kuwa msimamo wake wa maisha ni wa kukatisha tamaa. Hata hivyo, wengi wa wahakiki hao, kama vile Musau (1985), Mulokozi (1983), Senkoro (1982), Baru (1992) kwa kiasi kikubwa wamezitegemea kazi za awali za msanii huyu.

Senkoro ametoa kauli hii:

> Maisha kwa kufuatana na
>
> Euphraze Kezilahabi hayana maana
>
> Kwani ni tanzia tupu[4]

Katika sura hii tutaonyesha maana ya maisha kama ambavyo mwandishi ametusawiria katika novela hizi (*Nagona* na *Mzingile*). Tutachunguza ukweli unaodhihirishwa na maisha hayo. Anavyoyajadili masiala ya raha, ukweli na maana ya maisha yamemtenga Kezilahabi siyo tu kama mwandishi aliyekata tamaa (kama ambavyo imedaiwa) bali msanii mpevu na mwanafalsafa kuhusu masuala nyeti ya jamii ya ulimwengu. Masuala ambayo ameyajadili ni masuala ambayo yameandikiwa na wanafalsafa na waandishi kama vile Friedrich Nietzsche, Jean-Jacques Rousseau, Jean – Paul Sartre, Albert Camus, Martin Heidegger, Samuel Beckett n.k.

## 3:2 Maana ya maisha

Maisha ya binadamu yamesawiriwa kama dhihaka na kejeli Binadamu huwa hajui anakoelekea na kuwa ni kana kwamba yeye huanza safari anapozaliwa Ni sababu hii ambayo imempelekea mwandishi kutusawiria wasimulizi ambao wanajikuta mara kwa mara katika sehemu za ajabu ajabu na zingine za kutisha ilhali hawajui walifika vipi katika sehemu hizo Anasema hivi katika *Nagona* kupitia kwa msimulizi :

> YAELEKEA ilikuwa jioni, maana kulikuwa na mwanga hafifu wa dhahabu humo bondeni nilimokuwa. Sikumbuki kuona jua na sikumbuki kuona mtu mwingine karibu nami.(uk.1)

Anapoanza safari anasikia mtu akitembea lakini huyo mtu haonekani Anasikia watu wakisoma vitabu lakini hawaonekani Ni kama kejeli kwani anaposhikwa na kichomı anasikia vicheko kutoka karibu kila mti (*Nagona* uk.1). Mwandishi anaendelea kututhibitishia maisha kama kejeli kwa kutumia stihizai ya kicheko. Wakaguzi waliopewa jukumu na serikali kukagua viwanda vilivyokuwa vikifanya kazi kwa hasara walichekwa kwa dharau na walinzi waliokuwa wakivilinda viwanda hivi. Walinzi hawa wanawaona kama wajinga (*Nagona uk.22)* ilhali walikuwa wameteuliwa kufanya kazi hiyo kutokana na elimu na tajriba yao katika nyanja hiyo.

Hapo msimulizi alikuwa katika juhudi za kutatua migogoro ya kiuchumi ambayo iliendelea kuisakama dunia. Lakini walinzi wanawacheka na kuwaona kama wajinga kwani walielewa tangu fika kuwa juhudi za binadamu hazimpatii suluhisho la matatizo yake.

Msimulizi na wenzake wanafika kwa mfalme katika harakati zao za kumsaka paa[5]. Huko vilevile wanachekwa na kufanyiwa kejeli na wasichana waliokuwa wakiwachungulia vidirishani. Wasichana hao wanawarejelea kwa kinaya kama mashujaa huku wakiangua kicheko cha kejeli na dhihaka. Walijua tangu fika kuwa hawatafaulu katika juhudi zao za kuusaka ukweli kwani wanasema kuwa wamekuja kuzika mifupa yao (*Nagona* uk.29).

Hapa vilevile mwandishi anaonyesha maisha ya mwanadamu kama kejeli na dhihaka tupu. Juhudi zake za kusaka ukweli wa maisha hazimfikishi mbali kwani kama ambavyo wasichana wanavyosema watafikia tu kujifia. Maelfu ya watu wamewahi kufika katika sehemu hiyo wakiwa katika ari ya kutafuta ukweli lakini walifaulu tu kuyaacha mafuvu yao humo.

Kwenye diwani yake ya *Kichomi* (1974:34), msanii huyu anasema hivi katika shairi la 'Nimechoka' :

Ninaendelea kuning'inia Nimechoka Mikono
inaniuma; hatari ya vitimbo . Vinacheka.......

Lakini pole pole ninaanza kutabasamu.
Sijafika hatua ya kucheka ; maana nimechoka,
Kichomi kimenipata na sijadondoka

Hapo maisha ya mwanadamu yamesawiriwa kama mateso kwani kama asemavyo mshairi huyu amening'inia huku akiwa ameshikilia ncha za waya ngumu ya maisha. Lakini vitimbo vilivyo chini vinacheka huku vikimsubiri adondoke ili vimtoboe Ikifikia hapo pengine na yeye atafikia hatua ya kucheka. Hii ni kejeli na dhihaka kwani kutokana na ukatili na hatari zilizopo maishani mwa binadamu anachoweza ni kucheka tu, kwani hana uwezo.

Taswira ya maisha ya binadamu ambayo inapatikana katika novela hizi mbili ni maisha yenye hatari nyingi na katili. Ni sababu hii imempelekea mwandishi kutupitishia kwenye mandhari mbalimbali na safari zilizojaa vilinge na vitendawili Hofu inamshika msimulizi hadi kichomi kinaanza kumuuma ubavuni huku akisindikizwa na viboko matakoni (*Nagona* uk 1). Anajikuta kwenye mji wenye kimia ambacho kinatisha na nyumba zenye madirisha ambayo yanajifunga Hii ndiyo safari ya maisha ya binadamu. Msimulizi anasema hivi katika *Mzingile*:

....... kamwe usitegemee kuokota mkufu uliokamilishwa kwa ajili yako. Lazima usafiri utafute hivyo vipande ....(uk.6)

(Msisitizo wetu).

Safari yenyewe imejaa hatari kwani baadhi ya njia zimezibwa kwa miba. Aidha kukwea milima yenye majabali ambayo hayatachelea kukwangura magoti. Wale ambao waliaminika eti ndio walioshikilia ukweli walihitimu tu katika kuwekea njia madaraja yasiyoaminika. Na sauti iliokuwa ikitoka katika mwanga ilisema kuwa watu hawa ambao waliaminika kuwaongoza watu kwenye njia ya kweli walifaulu tu katika kuiwekea njia ngazi na madaraja yasiyoaminika (*Nagona* uk.15).

Wasomi na wanafalsafa wengi wamewahi kuliongelea suala la maisha ya binadamu lakini kulingana na mwandishi mafundisho yao yaliiwekea njia miba na madaraja yasiyoaminika.

Kuna vilevile miteremko mikali. Miteremko mikali kana kwamba ni maporomoko. Waaidha kuna mikondo mikali ya maji tayari kumzamisha atakaye dhubutu kuvuka (*Mzingile* uk 29-30). Hizi zote ni jazanda ainati alizotumia mwandishi ili kuonyesha hatari ambazo humkabili binadamu katika safari yake ya maisha. Kuna mitambo hatari ambayo binadamu mwenyewe amebuni na sasa inatishia maisha yake. Katika novela zote

mbili ajali za mitambo ya nyuklia zinatokea na kusababisha maafa yasiyo kifani. Mwandishi hapa ameonyesha hatari zinazomkabili binadamu katika maisha yake.

Taswira ambayo msanii huyu ametuchorea ni ya maisha kama ambayo yamejaa vurumai tupu. Ni kwa nia ya kutaka kuonyesha maisha kama vurumai akamshirikisha kila mtu katika vurumai wakati wa Ngoma Kuu, katika novela ya *Nagona*. Mwanafalsafa (aliyeongoza ngoma kwa utaratibu), wanasaikolojia, wanamapinduzi na kila mtu alishiriki katika vurumai na tunafahamishwa uwanja mzima ulikuwa umechacharuka na ikawa vurumai tupu (uk.59). Mwandishi ametumia fumbo la ngoma kuu kurejelea siku ambayo makundi mbalimbali yalitarajiwa kushirikishwa ili kutoa mwongozo wa maisha. Hakuna kundi lililofaulu kwani makundi yote yalishiriki katika vurumai.

Mwandishi anaona watu mbalimbali katika kazi zao wakichangia katika vurumai ya dunia. Ni kwa sababu hii akawashirikisha watu wote katika vurumai - wanafalasafa, wanasaikolojia, wanamapinduzi na waliokuwa watazamaji - wote walishiriki katika vurumai ambayo ilikuwa raha yenyewe.

Mwandishi anaona raha ya maisha kama ambayo inapatikana katika vurumai za binadamu. Na anaendelea kusema kuwa watu wengi katika ule

mji uliotawaliwa na kimya walikufa wakati wa vurumai Ni kejeli na kinaya kwani tunafahamishwa walikufa hali wakicheka (*Nagona* uk 62)

Hapa mwandishi anaonyesha maisha kama kejeli na ambayo yatabaki kumchezea binadamu Haya ni maisha katili kama ambavyo amedai katika diwani ya *Kichomi* (1974:34):

> Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
>
> Nionako kwa huzuni vifurishi maelfu vya dhambi
>
> Kisu maisha kafiri haya.......

Ugumu huu wa maisha umepigiwa mwango katika riwaya ya Kezilahabi ya*Kichwamaji* (1974:209) anaposema kupitia mhusika Manase:

> Picha hii inaonyesha jinsi maisha ya binadamu yalivyo magumu Ukitazama vizuri utaweza kuona picha ya mwanadamu ameshikwa kati ya mtego huu kama samaki....

Hii ni taswira ya mwanadamu akiwa mtegoni kama samaki Mtego alioko ndani ni mtego wa maisha Samaki ameshindwa kujinasua na anabaki hapo

mtegoni kwani hana uwezo Vivyo hivyo binadamu huwa hana uwezo juu ya maisha bali huishi kama yalivyo na matatizo yake.

Mandhari ambazo zimetumika katika riwaya hizi mbili zimedhihirisha maisha yenye huzuni na kuemewa kwa binadamu Katika *Mzingile* tunamwona msimulizi akijikuta katika mazingira ambayo hajui alifika vipi Mara yupo kwenye miteremko mithili ya maporomoko. Wakati anaposhika safari hajui aelekee wapi . ' Anasema kuwa alianza safari asubuhi na mapema wakati fikra zilikuwa bado kuchoka lakini ajabu ni kuwa hakujua hata aelekee wapi kwani hakuna aliyejua (*Mzingile* uk 6).
Hii ina maanisha kuwa katika juhudi za mwanadamu za kutafuta ukweli huwa hana uhakika na analotenda na hufuata dira ya silika zake.

Sehemu zilizogurwa na zenye upweke zimetumika kuashiria kuemewa kwa mwanadamu katika kusaka ukweli Katika novela ya *Mzingile* msimulizi anatambua kile kilichokuwa kijiji chake kimekwisha na yamebaki magofu tu Anaemewa na hajui atende nini na anaanza kutembea ovyo Vivyo hivyo na mwanadamu huwa hajui alipe jibu gani swali la ni nini maana ya maisha? Basi yeye hubaki tu kutapatapa hapa na pale kama nzi aliyeanguka majini

Maluweluwe na ukungu vimetumika kumwonyesha binadamu kama mtu aliye gizani – hali ambayo hutawala maisha yake. Mwandishi ametupitishia

kwenye mandhari ya bonde na tunakubaliana na M. Mbatia (1997:12) anaposema:

> Dhana ya bonde inazua picha ya mahali palipotawaliwa na giza ukungu, ukiwa na mauti. Bonde ni taashira ya ulimwengu ambayo inasisitiza kwamba ni mahali pasipofaa kwa kuishi.

Huu ndio ulimwengu mgumu ambao mwandishi ameusanii na binadamu anajikuta humo akiyaishi maisha hayo magumu

Ulimwengu ni mahala pabovu na pagumu kuishi. Mwandishi ametumia sitiari ya tambara bovu kuuweka ujumbe huu wazi Tambara bovu ukilivuta kidogo tu huraruka ovyo, lina ugumu wa kulitenda utakavyo. Na ndivyo mwandishi anauona ulimwengu. Ni mahali pasipofaa na ni vigumu kupaishi. Kupitia mwanamke anayechota maji mtoni msanii huyu amethibitisha ulimwengu kama mahala penye shida na ugumu mwingi Mwanamke huyu anasema kuwa ulimwengu ni tambara bovu na ni vigumu kuubeba (*Nagona* uk.24). Anajaribu kuubeba, anachoka, anakoga lakini hajawahi kufanikiwa. Mwanamke huyu anawakilisha juhudi za binadamu na jinsi ulimwengu umemwia vigumu.

Mwandishi hapa anaeleza jinsi ilivyo vigumu kuuelewa ulimwengu na jinsi maisha yalivyo magumu kwani ulimwengu wenyewe ni tambara bovu Ugumu wa maisha ya binadamu unaeleweka zaidi katika shairi lake la 'Mto nili' (*Kichomi* 1974 7) ambapo anaona maisha pekee ni adhabu tosha Anasema

> Ni adhabu ya kutosha kupaswa kuishi
> juu ya sahani yenye joto kali, ya kukaangia
> Na yaliyopita, yamepita.

Sitiari ya dunia kama sahani ya kukaangia na yenye joto kali imefikisha ujumbe aliolenga mwandishi Kwa Kezilahabi maisha ya binadamu ni kama kuwekelewa kwenye kikaango hiki chenye joto kali – adhabu kali hii!

Ili kuwekea tashuhuda kwamba maisha ya binadamu ni adhabu iliyoshinda mambo mengine yoyote anayokumbana nayo, katika riwaya yake *Kichwamaji* (1974 94) kupitia mhusika Kazimoto mwandishi anasema kuwa kutunza maisha yake ndiyo adhabu ambayo kila mwanadamu amepewa Ni adhabu kwani maisha yenyewe hayashibishwi wala hayaridhishwi.

Hii ni kumaanisha kuwa kuyaishi maisha yake ndiyo adhabu kali aliowahi kupata binadamu Adhabu ya maisha ni sawa na ya mtu anayesukuma jiwe

kuelekea kilele cha mlima, mara tu anapokaribia kulifikisha huko – linabingirika na kurejea chini tena. Mhusika Sysyphus anaanza tena kulisukuma kama ambavyo imeelezwa na Cruickshank (1958:15). Kezilahabi ameyasawiri maisha yakiwa magumu kutokana na hali ngumu ya kiuchumi na kisiasa ya nchi yake na ya mataifa ya ulimwengu wa tatu kwa jumla (tazama sura ya 4 ya tasnifu hii).

Hoja nyingine muhimu ambayo imejidhihirisha katika novela hizi ni kuwa binadamu hana hiari na matukio ya maishani mwake na takriban huwa ni kama ajali. Awali kabisa ni kuzaliwa kwa binadamu. Yeye huwa hana hiari na tukio hili na takriban huwa ni ajali kwake. Katika novela ya *Nagona* babu na msimulizi wanajibizana hivi:

> "Hapana. Nataka tu kujua habari za kuzaliwa kwangu. Wazazi wangu hawajapata kunieleza kikamilifu".
>
> "Ulifika wakati ambapo ajali ilikuwa lazima itokee. Ajali hii ilitokea katika bonde la hisia ......" (uk 11)

Asili ya maisha ya mwanadamu ni kitendawili kigumu kulingana na mwandishi na hakuna anayekielewa. Ni kama ajali tu ambayo ni lazima itokee. Kwa jumla mwandishi ameyasawiri maisha kama kitendawili

ambacho hakina jibu Kuhusu suala la maisha binadamu huwa kama mnyama asiyejua zuri wala baya Ili kudhirisha hoja hii babu anamwambia msimulizi kuwa kabla ya kuzaliwa kwake hakuna aliyejua lililopaswa kufanywa - hakuna aliyetambua zuri au baya (*Nagona* uk 11)

Maisha ya binadamu yamegubikwa na giza la kutojua kama ambavyo imedhihirika kupitia mwandishi huyu. Hii imewekwa bayana kupitia wahusika ambao mara kwa mara wanajikuta wamepotea njia na katika sehemu ambazo hawajui walifika vipi. Hapa mwandishi anaelekea kutetea dhana kuwa mwanadamu huwa hana uwezo wowote na hufuata matukio katika maisha yake kwa hisia tu Hasa katika *Mzingile* mhusika anaanza safari ya kwenda kwa Mungu lakini hakujua hata aelekee wapi. Njiani anakuta njia panda na hajui afuate njia ipi. Anwani ya novela hii imetumika kama sitiari kuwakilisha mtu aliyezongwa na msokotero wa viroja. Katika *Nagona* vilevile msimulizi anaanza safari ya kumsaka paa lakini mara kwa mara nyayo zinampotea asijue zimepotelea wapi Taswira ya kutafuta nyayo za paa huyu nyikani penye majani marefu ni tosha kubainisha mwanadamu alivyoemewa

Kezilahabi ana yaona maisha kama ndoto tu. Kama vile ambavyo hakuna ukweli katika ndoto na katika maisha vilevile hakuna ukweli. Suala hili la ukweli tutalirejelea baadaye na kulijadili kwa kirefu. Katika *Mzingile* mhusika mkuu ameonyeshwa akiwa katika ndoto za ajabu ajabu

kumaanisha ukweli wa maisha yake haupo na kwamba maisha yenyewe ni ndoto tupu. Hata inakuwa vigumu kupambanua kati ya ndoto na hali halisi Anasema hivi (*Mzingile* uk 17):

> Daima nilitaka kuwa kichaa. Lakini akili timamu ziliniusia. 'Usiwe!' Nilitamani sana kuogelea katika bahari ya nusu urazini, kati ya kuwa na kutokuwako, kati ya ndoto na hali halisi....

Inakuwa muhali kupambanua kati ya ukweli unaodhihirishwa na maisha na ndoto. Katika *Nagona* dhana hii imejitokeza wakati mhusika mkuu anasema watu wengine hawakupata nafasi katika uwanja wa ngoma. Siku kabla ya ngoma , kwa ajili ya wasiwasi mkubwa waliokuwa nao, walitumbukia katika kisima cha ndoto zao (*Nagona* uk.62) Binadamu ameonyeshwa akiishi maisha ya wasiwasi na ni katika ndoto tu ambapo anaweza kuona maana ya maisha yake.

Basi Kezilahabi anayasawiri maisha kama mzaha na yasiyo na maana. Hususan huwa hakuna ukweli katika ndoto. Wakati mwingine ndoto fulani hutokea kuwa kweli, lakini kwa nadra sana Msanii huyu anaonelea ni afadhali ndoto kuliko maisha kwani wakati fulani ndoto fulani yaweza ikatokea kuwa kweli. Katika *Mzingile* (uk 12) mzee anadai kuwa amesahau mengi kwani anatumia muda wake mwingi katika kuota

Anasema kuwa ndoto ni tamu kuliko maisha na halisi kuliko uhalisi wa maisha Basi kulingana na Kezilahabi heri ya ndoto kuliko maisha kwani ndoto huweza kuwa na uhalisi ilhali maisha yenyewe hayana uhalisi

Maisha ni kama mzaha na ndiyo sababu yanaweza kuishika Ni kama stihizai kuyaishi maisha na maisha yenyewe ni mchezo Ni katika kuona maisha kama mchezo ndiyo mwanadamu ataweza kuyaishi Katika *Mzingile* (uk.13) mzee anasema:

> Maisha yenyewe ni mzaha mkubwa kuliko yote
> Ndiyo maana yanaweza kuishika

Msanii huyu anaona kifo kama hatima ya maisha ya mwanadamu ambaye hukiogopa mno Lakini mpaka wenyewe baina ya kifo na uhai haupo kwani mwanadamu huendelea kufa tangu alipozaliwa Binadamu hapaswi kuogopa kifo kwani hukamilisha tu safari ndefu na ngumu, katika *Mzingile* (uk.14) mzee anaendelea kutongoa, anasema

> Kama unaogopa kufa kaa kimya urejeapo Lakini kumbuka ujasiri wa mja hukamilishwa na kifo.

Mwandishi anakitazama kifo kama ambacho kitadhihirisha ushujaa wa binadamu baada ya kumaliza adhabu ya maisha katika ulimwengu katili

Binadamu hapaswi kuogopa kifo kwani kitadhihirisha ushujaa wake Utakuwa ni ushujaa kwani atakuwa ameshinda adhabu kubwa ya zote alizopewa – ya kutunza maisha yake. Binadamu hapaswi kuogopa kifo kwani ni moja ya hatua zake za maisha Kuogopa kifo ni aibu kama ambavyo kipofu anamfafanulia msimulizi kuwa binadamu ni waoga sana kwani wanajenga majumba marefu na kuruka angani lakini wanangoja vijidudu vidogo tu vya malaria ili viwaondolee aibu ya woga (*Mzingile* uk.29).

Kwa maoni ya Kezilahabi basi hakuna mpaka bainifu baina ya kifo na uhai na basi binadamu hapaswi kuogopa kifo. Hapaswi kuogopa kifo kwani ni kifo ambacho kitadhihirisha ujasiri wake. Basi kwa misingi ya madai haya, ikiwezekana binadamu ayaondoe maisha yake mwenyewe.

Mtazamo huu unaoana na wa wale ambao hutetea falsafa ya udhanaishi Kulingana na Albert Camus ambaye ni mashuhuri wa tapo mojawapo la falsafa hii:

> Kifo kinaweza kuleta maana katika maisha katili na
> yasiyo na maana.[6]
> (Tafsiri yetu)

Kama ambavyo imedhihirika hapo awali maisha hayana maana kwani yametwaliwa na ukatili na vurugu Basi ili kuleta maana katika maisha ya namna hii mwanafalsafa huyu anatoa suluhisho la kifo Kama Camus mwandishi haoni tofauti kubwa baina ya maisha na kifo Ni kana kwamba vyote hukamilishana Suala hili linaonyesha jinsi Kezilahabi alivyoathiriwa na kazi za wadhanaishi Dhana hii ameielezea bayana zaidi katika *Kichwamaji* (uk. 206), mhusika Manase anaposema kuwa ukweli ni kwamba sisi wanadamu tunakufa polepole. Imani ya watu kuwa kifo kinatokea mara moja ni potovu Kwa hivyo kulingana na msanii huyu tangu mwanadamu anapozaliwa anaanza kufa polepole ingawa yeye anajiona yuko sawa. Tangu anapozaliwa siku zake zinaondolewa moja moja na kaburi ni hatua ya mwisho tu. Kama ambavyo tumedai hapo awali mwandishi haoni tofauti baina ya uhai na kufa kwani ikiwa ni kwamba tunapoishi tunakufa polepole basi kufa ni kuishi. Na ikiwa kufa ni kuishi hakuna mpaka baina ya maisha katika uhai na baada ya kufa.

Hii ni dhana nyingine muhimu ya udhanaishi Maoni haya ya Kezilahabi ni sawa na ya mwanafalsafa mashuhuri wa mwegemeo huu, Samuel Beckett, ambaye anadai:

> Maisha ni kuendelea kufa, mfanyiko ambao unaendelea mpaka kiwango kitakiwacho – kifo cha hakika.[7]

(Tafsiri yetu)

Ikiwa mtu aliyekufa ni sawa na anayeishi basi maisha hayana maana yoyote. Binadamu huwa hana maana yoyote baada ya kifo kwani siyo binadamu tena bali maiti. Tutajadili jinsi mtazamo wa mwandishi ulivyoathiriwa na wanafalsafa wa udhanaishi katika sura ijayo.

## 3:3 Kukosa furaha kwa maisha ya mwanadamu

Hisia za huzuni zinatujia tunaposoma maafa mbalimbali katika novela zote mbili. Katika *Mzingile* msimulizi amesema hivi :

> ....... Karibu na mifupa hii niliona karatasi ngumu iliyokuwa imeandikwa maneno yafuatayo:
>
> *Kwa yeyote awaye*
> *Nilikuwa wa mwisho kufa*
> *Katika tarafa hii* (uk 55)

Huu ni ujumbe wa kuhuzunisha kwani kila mtu ameangamia na uhai ambao umebakia ni mimea peke yake. Mwandishi ametumia dhana ya kifo kuonyesha huzuni na kusikitika kwa binadamu. Kifo husikitisha na kuhuzunisha mtu yeyote awaye. Maisha yaliyotawaliwa na kifo kamwe

hayatakuwa na furaha. Vilevile katika novela ya *Nagona* tunahuzunika wakati mwandishi anatuchorea taswira ya vurumai wakati wa ngoma kuu. Watu walikanyagana, kusukumana na kuumizana. Anasema kwamba, "Hiyo ndiyo ilikuwa raha yenyewe" (uk. 59). Watu walishikwa na vichomi na wengi wakafa. Binadamu anashindwa kulitatua swali hili gumu na mwandishi akamgubika mazingira ya huzuni. Haya ndiyo maisha ya binadamu.

Toni ya huzuni, ambayo imetawala katika kazi hizi za mwandishi huyu, imetumiwa kuonyesha kulemewa kwa binadamu katika suala la maisha. Toni hii inaonyesha kuwa maisha ya binadamu hayana furaha hata kidogo. Binadamu anapokabiliwa na baa au mkasa wowote, yeye huwa hana uwezo na hushtakia hali yake kwa Mungu. Hata anapokabiliwa na kifo yeye huwa hana uwezo. Msimulizi anasema katika *Mzingile* kuwa siku moja mlima ulichachamaa na kutoa moto mwingi uliofurika toka juu hadi chini kama tope zito la moto. Janga hili lilipowakabili, watu hawakuwa na la kufanya ila walimwendea Kakulu ili atulize hasira zake. Hii ni sawa na binadamu kumwendea Mungu anapokabiliwa na baa lolote.

Dhana ya maisha ya binadamu kutokuwa na furaha imejitokeza katika kazi zingine za Kezilahabi. Kwenye riwaya ya *Kichwamaji* mhusika Kazimoto anasema:

> Mwanadamu ni kiumbe ambaye amejaribu kutafuta njia nyingi zitakazomwezesha kupata furaha Kwa kuwa ameshindwa kupata furaha hapa duniani amejenga kichwani mwake kitu kama mbingu, yaani mahali anapotegemea kupata furaha baada ya kufa. (uk 137)

Basi ina maana kuwa shughuli nyingi za binadamu huelekezewa katika kutafuta furaha katika ulimwengu katili. Lakini mwandishi anaelekea kusema kuwa binadamu hatawahi kuipata hii furaha Baada ya yeye kushindwa kupata furaha duniani amejenga imani kichwani mwake kuwa furaha itapatikana mbinguni Wakristo wanaamini kuwa furaha itapatikana baada ya kifo – paradiso Mawazo haya yameona na ya Albert Camus anayedai kuwa furaha ya kudumu haiwezi kupatikana katika maisha ya binadamu, Cruickshank (1958 27).

Kezilahabi ametusawiria ulimwengu kama mahala pasipo na furaha na ambapo maafa ya kila aina yamestawi Awali kabisa binadamu anajimaliza mwenyewe kutokana na elimu yake Anatengeneza zana na mitambo hatari kwa maisha yake Bomu la nyuklia linaangushwa na watu wanakufa kama panya na wanaosalia wanadhoofu Msimulizi anaelezea kuwa bomu la nyuklia lilidondoshwa na mataifa yaliyoanza kutupiana zana hizo na watu walikufa kama panya (*Mzingile* uk 45).

Hii ni taswira ya ulimwengu ambayo inatuonyesha dunia kama pahala pasipofaa na mahala pa hatari kubwa. Watu wengi kupita kiasi wanakufa, mwandishi anawafananisha na jinsi panya wanavyokufa. Siyo kufa tu, wanaobaki wanadhoofu kiasi cha kutoweza kujichimbia makaburi yenye kina cha kutosha.

Ajali mbalimbali zinatokea na kumwangamiza binadamu. Hasa katika *Nagona* motifu ya ajali imetumika kutudhihirishia kuwa binadamu hana chochote ambacho anaweza kujipangia. Matukio yote maishani mwake ni ajali tu. Hali hii ni ya kusikitisha kwani mbali na juhudi zote za binadamu dunia ina hali yake ya kujiendeshea mifanyiko yake. Hata kifo cha binadamu ni ajali tu. Katika *Nagona* kizee kinasema hivi:

> .....Katika bonde hili kuna imani kuwa ajali ni mwanzo tu wa kitu au wazo jipya. Bila ajali hakuna ambacho kingekuweko. Kuzaliwa kwenu ndiyo ajali kubwa iliyopata kutokea katika uhai wenu...... Je, hamkumbuki kwamba ajali ndiyo iliyowafikisha hapa haraka! (uk 23)

Nukuu hii imetudhihirishia kuwa kwa maoni ya mwandishi hakuna chochote ambacho binadamu anaweza kujipangia na hata ubunifu na ugunduzi wake ni ajali tu.

Ubunifu na ugunduzi wa binadamu unakuwa ajali kwani uvumbuzi wenyewe unasababisha kuangamia kwake. Hata viwanda vyake vinakuwa tishio kwa uhai wake. Hii ni kuonyesha dunia siyo mahala pa salama. Viwanda hivi vinatoa sumu kali. Hata vinatumika kutengeneza zana hatari za nyuklia ambazo zinasababisha maafa makubwa. Kuhusu viwanda hivi Kizee kinasema hivi, "Hayo ni baadhi tu ya mambo yanayoifanya siku ya Ngoma Kuu kufika upesi" (*Nagona* uk.23). Viwanda hivi vinamfanya binadamu akaribie kifo chake haraka kwani vinatoa maji yenye sumu kali ambayo kama kizee kisemavyo, yatasababisha maafa.

Mahala palipotawaliwa na ajali na matukio ya kutisha uhai hapawezi kuwa mahala pa furaha. Taaluma za binadamu zinavuruga utulivu wa dunia na ndizo ambazo pengine zitaleta mwisho wa dunia. Taaluma zote zinakuwa kama ajali kwani binadamu anashindwa kudhibiti matokeo na mambo yanayosababishwa na taaluma hizi.

Furaha ni kitu ambacho mwanadamu kamwe hataweza kukishika. Dhana hii imejiweka bayana zaidi katika riwaya yake ya *Dunia uwanja wa Fujo* (1975:163). Mhusika Dennis anamwambia Tumaini:

> Tumaini la furaha ni wazo tu ambalo linaweza kusukuma mwanadamu mbele ili kumwangamiza ama kumuendeleza. Lakini hatalishika mkononi

Kwa maoni ya mwandishi basi furaha ni wazo tu wala siyo hali ambayo mwanadamu ataifikia.

Mwandishi ameonyesha siasa kama chanzo cha balaa katika ulimwengu uliokuwa shwari na mtulivu. Msimulizi anasema kuwa watu walikuwa na moyo wa kujitolea na kushirikiana na katika hali hii kulikuwa na matumaini. Lakini kulitokea balaa ya viongozi kutaka sifa kwa yote yaliyotokea (*Mzingile* uk.44).

Watu walikuwa na umoja na kushirikiana katika kujitolea ili kujiendeleza. Lakini kama ambavyo mwandishi ametusawiria hali ya dunia, bila furaha, mara kunatokea balaa. Mwandishi hapa anamithilisha siasa na balaa kwani inawafanya watu vikaragosi vya kuwasifu viongozi.

Viongozi wa siasa wamesawiriwa kama wenye kuchangia matatizo ya ulimwengu na kuwa nguzo ya ukosefu wa amani na furaha. Mwandishi anasema kuwa wanawaongoza watu kwenye vichochoro vya uchumi

vilivyoacha kutumika zamani. Wanawafanya hata wataalamu vikaragosi vyao (uk.44). Matokeo ya haya yote ni kusambaratika kwa uchumi na kushuka kwa thamani ya pesa. Hii inapelekea kuchafuka kwa nchi kutokana na migomo ya wanafunzi ambao wanakomeshwa kwa virungu.

Uchafuzi huu wa nchi unafikishwa kileleni na ufisadi na unyakuzi wa kidogo kilichoko. Mwandishi anatumia sitiari mwafaka ya jahazi baharini na anasema, "Katika kuyumbayumba tukagonga mwamba wa kwanza". Isitoshe, sitiari inayolenga ndipo ni ya kuziba ufa kwenye jahazi kwa pamba. Hili ni suluhisho la muda kwani kuziba ufa kwa pamba ni kumaanisha kuwa maji yataendelea kulowanisha pamba hiyo na hatimaye kuvuja ndani. Msanii hapa anaonyesha kuwa utatuzi wa shida zilizopo na wanasiasa ni wa muda mfupi tu na hali hurejelea kama awali-chombo huendelea kuzama. Matatizo ya binadamu huendelea kumsakama na hata kumzamisha penye maji marefu zaidi. Mwandishi anatetea dai kuwa wanasiasa hawatatatua shida za binadamu. Ebrahim (1971:21) vilevile ametumia sitiari ya jahazi kurejelea nchi changa za Afrika baada ya kujipatia uhuru.

Badala yake wanaacha jahazi liendeshwe na upepo. Juhudi za binadamu za kuendesha nchi basi zinashindwa na basi anaendeshwa na majaaliwa. Watu wanaambiwa wasichague chakula, wale chochote kilichopatikana ilhali viongozi wanawania vyeo katika serikali. Katika hali hiyo furaha

inakosekana na inakuwa ni vurumai tupu – mahali pasipofaa Msimulizi anasema hivi katika *Mzingile*.

> ..........cha kugawana kilipopungua pakatokea miongoni mwao ugonjwa wa kuwania vyeo katika chama na serikali Pakawa na mbinu za kuondoana njiani. Ikawa vurugu tupu. (uk.45)

Hapa mwandishi anasawiri dunia kama mahali pa vurumai tupu. Vurumai hizi hazikomi kwenye fujo pekee bali hata kuuana kupo ili mtu apate anachokitamani - vyeo katika chama na serikali. Huu ni ubarakala na ubinafsi uliovuka mipaka.

Utashi wa vyeo na mamlaka haukomi katika vurumai tu, bali kama ambavyo tumedokeza hapo juu kuna kuuana ili binadamu avipate vitu hivi viwili Hiki ndicho kisababishi kimoja cha dunia kuwa vurugu na vurumai tupu kama ambavyo mwandishi amefafanua kwenye novela ya *Nagona*. Msimulizi anamwambia padre kuwa ameshiriki katika mauaji ya watu wanne kwa kulipa watu fedha ili watekeleze kadhia hiyo (*Nagona* uk.48)

Binadamu anatekeleza mauaji ya kisiasa kutokana na utashi wa vyeo na anasa Wanasiasa basi wanachangia katika kuchafua dunia na kuwa moja ya kisababishi cha kutokuwepo kwa furaha duniani. Dunia inakuwa ni mahala

pa fujo ya kuondoana kutokana na ubinafsi na utashi wa kisiasa. Huu ndio mchango wa wanasiasa katika kuuchafua ulimwengu. Kama nadharia ya kisosholojia ambavyo husisitiza mazingira ambamo kazi ya kisanii huibuka ni muhimu katika kuihakiki kazi ya kisanii. Vurugu hizi za kisiasa ambazo mwandishi ameziongelea ni hali halisi ambazo hutokea katika ulimwengu wa tatu (tazama sura ya IV ya tasnifu hii).

Mwandishi anaendela kusema kuwa hata haki haiwezi ikatekelezwa. Mhusika mkuu katika mauaji hapelekwi kortini na wale ambao wanapelekwa huko wanahukumiwa miezi kadhaa tu (*Nagona* uk.49). Haki inazuiliwa kutendeka kutokana na ufisadi. Ni ajabu kwani mtuhumiwa mkuu katika mauaji ndiye kizingiti katika kuhakikisha kuwa haki haitendeki kwa kutoa rushwa. Mahakimu nao wako tayari kupokea hongo ili wabatilishe sheria. Hali hizi zinashuhudiwa nchini Tanzania na nyingi ya mataifa katika ulimwengu wa tatu.

Dunia haina furaha kutokana na matatizo tumbitumbi yanayoitawala. Binadamu naye ameshindwa kuyadhibiti matatizo haya. Matatizo haya ni pamoja na janga la ukame ambalo linasababisha ukosefu wa chakula na basi kumtia binadamu katika hali mbaya ya njaa. Uwezo wa binadamu unafikia mwisho na anaanza kutoa kafara chini ya mibuyu ili kumtambikia Mungu (*Mzingile* Uk.4). Mwandishi ametuchorea dunia ambayo imekereka na

kiangazi hadi kufikia hatua ya binadamu kumla binadamu mwenzake ilhali wengine wanakula panzi na mijusi. Hii ni hali ya kusikitisha mno.

Mwandishi ameusawiri ulimwengu kama ambao unaelekea kutikisika mhimili unaoushikilia kutokana na ukosefu wa sifa muhimu ambazo zingeufanya mahala bora. Huu ni ukosefu wa wema, imani na upendo. Badala yake panakuwa na hali ya wasiwasi na ukosefu wa amani. Msimulizi anasema hivi katika *Mzingile:*

> ......palikuwa na ukame uliotawaliwa na hofu ya kufa na kutoweka kabisa kwa taifa la binadamu. Palikuwa na ukame wa wema, ukame wa imani na upendo na ukame wa fikira. Palikuwa na uwingi wa choyo, kiburi, uonevu, ubinafsi, ubarakala na maasi....(uk.5)

## 3:4 Dhana ya ukweli

Tangu mwanzo hadi mwisho novela hizi mbili, *Nagona* na *Mzingile*, zimeonyesha juhudi mbalimbali za binadamu katika kutafuta ukweli. Huu ni ukweli unaozingira dunia yake na maisha yake kwa jumla. Katika *Mzingile* ukweli huu umewakilishwa na sitiari ya mwanamke mrembo

ambaye inakuwa ni muhali kumpata. Vilevile mwanga umetumiwa na mwandishi hapa na pale ili kuwakilisha dhana ya kufichua kilichojificha. Katika *Nagona* ukweli umewakilishwa na sitiari za paa, mwanga na Nagona.

Katika novela zote mbili mwandishi amedhihirisha kuwa kama katika furaha, ukweli vilevile hauwezi ukapatikana. Katika *Mzingile*, msimulizi anaongozwa na mwanamke katika safari yake lakini kila anapotia bidii kumfikia ndivyo umbali kati yake na yeye unavyozidi kuongezeka.

Ugumu wa kuupata ukweli binadamu anaoutafuta umejidhihirisha. Katika *Mzingile* inambidi msimulizi kupanda vilima na kuteremka miteremko mikali. Hata anapitia sehemu zenye mchanga mwingi ambao unarudisha nyuma nyayo zake. Njia ni yenye miiba na inambidi alale nje katika safari yake ya kusaka ukweli.

Aidha katika *Nagona* ugumu wa kumfuata paa umedhihirika. Kuna kupanda milima na kushuka, kuvuka mito na misitu mikubwa. Waaidha msimulizi anafuata nyayo tu kwani hata paa mwenyewe haonekani. Inakuwa ni muhali zaidi kufuatilia nyayo za paa katika nyika yenye majani marefu. Mara nyayo zinapotea sehemu fulani fulani na hawazioni. Wanapofika kwa mfalme wanapewa mitihani migumu ambayo kama wangeshindwa wangeuawa.

Katika novela hizi mbili Kezilahabi ameliweka bayana suala la ukweli - kwamba haupatikani. Baada ya msimulizi (wakiwa na wenzake) kufaulu katika mitihani migumu wanapewa paa, ambaye anatokea kuwa msichana mrembo. Wanaamua kupigana mieleka na msichana huyu ili akimshinda awe wake. Lakini msichana anamshinda na kutoweka kumaanisha kuwa ukweli umemkwepa tena. Mhusika mkuu anasema kuwa alishikwa kwa nguvu na msichana huyu akainuliwa na kutupwa chini kama gunia shida. Alichukua (msichana) nguo zake na akiwa amelala chini aliweza kuona akiruka milima halafu akatoweka (*Nagona* uk.38).

Hii inamaanisha binadamu amepigwa mweleka na ameangushwa na ukweli tena. Pale ambapo anafikiria ameupata ukweli ndipo unapomkanganya na kumpotea huku akibaki gizani kama awali. Katika *Mzingile* msimulizi anasema:

> ...... Nilitembea harakaharaka kuelekea hapo nikimeza mate mara mbilimbili. Nilipomkaribia nilimrukia juu kumkumbatia na kumpapasa hali nikisema kwa sauti "Nakupenda! Karne na karne nikikutafuta wewe !" (uk 8)

Tangu jadi mwanadamu amekuwa akitafuta ukweli. Amekuwa akifanya kila juhudi ili kupata ukweli unaozingira ulimwengu wake Lakini kama tulivyokwisha dokeza ukweli huu haupatikani kwani anaendelea kusema

> Pale nilipoangukia hapakuwa na mtu Palikuwa na mchanga uliokuwa kama tuta. Hakuna nilichoshika, isipokuwa mchanga........ (ibid)

Ukweli unawakilishwa na mwanga kwenye kitovu cha duara Lakini haufikiliki. Watu wamebaki tu kuzunguka kwenye duara zao bila kufikia katikati penye mwanga Hata katika vurumai zake binadamu ameshindwa kufikia kitovu cha duara penye mwanga Katika novela ya *Nagona* tunaambiwa kuwa msimulizi alijikuta anakokotwa na mkondo wa utashi kufuata duara. Lakini alizidi kuyakazia macho katikati kwani hangeweza kupafikia (*Nagona* uk.61-62). Katikati ya duara ndipo penye mwanga unaowakilisha ukweli.

Sitiara ya nagona kama kiwakilishi cha ukweli na uhalisi wa maisha ya binadamu imedhihirisha vilevile kuwa haupatikani Lakini binadamu hutia ghera katika kumsaka lakini kila mara akimpinga chenga. Katika *Nagona* babu anasema kuwa katika uhai wake wote Nagona alimpiga chenga Ni mara nyingi alimwona kwa mbali na mara chache sana alikaribiana naye kwani kila alipomkaribia alirudi kinyumenyume huku naye akiendelea

kumfuata (*Nagona* uk 44) Binadamu basi anatia kani na bidii kufuata ukweli huu maishani mwake lakini ni muhali kuutia mikononi mwake

Ukweli binadamu autafutao hajawahi kuutia mkokoni, anapoukaribia unarudi kinyumenyume na anapoushika anamponyoka Hata katika kumsaka huyu nagona hana hiari kwani anaendelea kufuata tu huku akiongozwa na nguvu fulani

Binadamu hatapata ukweli. Katika kumsaka Nagona kuna hatari na kila wakati binadamu anapofikiria amempata ndiyo hamu ya kuendelea kumwona inavyozidi Hii ina maana kuwa hatowahi kumfahamu kwa ukamilifu Anamvutia (Nagona) binadamu kisha anaambaa Ndiyo sababu babu akasema :

> ......Lakini ajabu ni kwamba unavutwa kumtazama bila kinga licha ya hatari zake Ukishamwona hamu ya kuendelea kumwona haiishi..... utajikuta unavutwa kuelekea kwake Lakini hatakuruhusu umshike awe wako peke yako, maana ni wa kila mtu Kila mtu anamtambua na ndiyo maana anavuta na anaambaa, sisi tunavutika na tunamwambaa ....... (*Nagona* uk 45).

Sifa moja ambayo imepewa ukweli ni utelezi Utelezi huu unaufanya ukweli uepuke juhudi kubwa za binadamu za kuushika na kuufanya wake Sifa hizi zimepewa paa ambaye alikuwa akisakwa na msimulizi na wazee waliofaulu katika mitihani ya kumpata (anawakilisha ukweli). Wanapopigana mieleka msimulizi anasema alijaribu kumshika lakini alikuwa hashikiki kwani mwili wake ulikuwa unateleza Alipojaribu kumuinua alikuwa na utelezi mwingi vilevile (*Nagona* uk 38).

Binadamu basi anashindwa na kumdhibiti na basi anamtoroka Kama tulivyokwisha sema msichana huyu anawakilisha ukweli na binadamu basi anashindwa kuudhibiti ukweli na anabaki katika kilinge cha mambo kama ilivyokuwa awali

Kezilahabi ameegemea vikubwa falsafa ya udhanaishi katika kulijadili suala la ukweli. Nadharia ya kisosholojia husisitiza kuwa maisha ya mwandishi ni suala muhimu ili kuweza kuihakiki kazi ya kifasihi Kwa kufungamana na kauli hii tunaweza kurudi nyuma na kuona uasili wa mawazo yake katika kazi za wadhanaishi kama vile Soren Keirkgaard (tazama sura ya 4)

Msimulizi anaposhindwa kumdhibiti paa, mwandishi analiona hili kama ni anguko la pili. Mwenda Mbatiah (1997:14) analiona anguko la kwanza kama ambalo limeelezewa katika Biblia Takatifu na Qurani Takatifu wakati

Mungu alipovunja uhusiano wake na Adamu na Hawa baada ya wao kutenda dhambi. Na basi anasema hivi kuhusu anguko la pili:

> .....Katika muktadha huu, anguko la pili ni kushindwa kwa mwanadamu kwa mara ya pili katika mtihani wa kuyapa maisha yake maana na mwelekeo.....

### 3:5 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili maana ya maisha ya binadamu kupitia jicho la mwandishi. Tumeona vile ambavyo mwandishi ameyasawiri maisha ya binadamu yakiwa taanzia na vurumai tupu. Aidha tumeona vile ambavyo maisha ya binadamu yalivyo kama kejeli na dhihaka kwake yeye mwenyewe kwani ameshindwa kuyaelewa. Waaidha katika kujaribu kuyaelewa anakabiliwa na hatari mbalimbali ambazo zinatishia uhai wake. Katika juhudi zake mbalimbali binadamu amedhihirisha hana hiari na matukio mbalimbali maishani mwake na ni kama ambaye anafuata nguvu fulani inayomzungusha katika duara ya maisha yake. Mtazamo huu unawakilisha maoni na falsafa ya mwandishi kuhusu dhana ya maisha ya binadamu ulimwenguni. Hata hivyo, mtazamo wa mwandishi umeathiriwa na mazingira na waandishi mbalimbali wa kidhanaishi. Kwa kufungamana

na nadharia ya kisosholojia tutayajadili masuala haya kwa kirefu katika sura inayofuata

Aidha tumelitalii suala la furaha na upeo wake Kwa muktadha huu mwandishi amebainisha kuwa haamini kama ulimwengu ni mahala ambapo panaweza kuwa na furaha Badala yake ni mahala penye maafa na kwa maneno yake "furaha ni wazo tu ambalo linaweza kusukuma mwanadamu mbele". Tumeona vile ambavyo harakati za kisiasa na wanasiasa pia wamechangia katika kuvuruga amani ya dunia na badala yake wakaleta mbinu za kuondoana Hizi ni athari za kisiasa na kijamii ambazo msanii amezipata kutoka kwa jamii yake (tutalijadili suala hili vilevile kwa kirefu katika sura ya 4)

Hatimaye tumechunguza dhana ya ukweli kama ambavyo imejidhihirisha katika novela mbili tunazohakiki Tumeona vile ambavyo binadamu yumo mbioni akijaribu kusaka ukweli Ukweli nao unamkwepa na utelezi wake haumruhusu audhibiti. Ukweli unampiga chenga hapa na pale na anapoukumbatia unampiga mweleka na kumwangusha kisha unatoweka Basi binadamu hatoupata ukweli Katika sura ifuatayo tutachunguza jinsi mwandishi alivyoathiriwa na waandishi mbalimbali na mazingira yaliyoizaa kazi yake, kama ambavyo nadharia ya kisosholojia husisitiza.

## TANBIHI

[1] Baru, T. W, (1992) : Tasnifu ya M.A

[2] Michira, J.N. (1991) : Tasnifu ya B. Ed

[3] Gatare, J. K (1993) : Tasnifu ya M.A

[4] Senkoro, F. (1982) : Fasihi, Publicity Press Centre, Dar es saalam, Uk. 89

[5] Wamitila, K.W.(1993) anaeleza paa kama fumbo lenye maana ya uhalisi, ukweli na maarifa Kezilahabi's Metaphysics. Kiswahili, Jarida la T.U.K.I., toleo 58, uk.3

[6] Katika Freeman E, (1971), The Theatre of Albert Camus (A critical Study), Methuen and co., London Uk.5

[7] Katika Mueller R.W. (1964) The Testament of Samuels Beckett, Faber and Faber, London, uk.110

[8]Sitiari inayowakilisha Mungu

# 4:0 SURA YA NNE

## 4:1 Utangulizi

Mtu haandiki katika ombwe tupu chambilecho Shaaban Robert[1] Aidha nadharia ya kisosholojia husisitiza kuwa mhakiki hawezi kuihakiki kazi ya fasihi bila kuzingatia mazingira yaliyoizaa kazi hiyo Haya ni mazingira ambamo msanii wa kazi husika hujikuta. Mazingira hayo yatakuwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii Maisha ya mwandishi vilevile ni muhimu ,hasa maisha ya shule na jinsi alivyoathiriwa na mitazamo ya wasomi mbalimbali.

Ni katika muktadha huu basi tutachunguza kuathiriwa kwa mwandishi katika sura hii. Ni athari mbalimbali maishani mwa Kezilahabi zilizompelekea kutunga kazi za aina yake na ambazo tunazihakiki - *Nagona* na *Mzingile* Aidha matamanio yake, kufaulu au kutofaulu kwake na kwa jamii yake maishani kumeathiri aina ya kazi ambayo ametunga kwa jinsi moja au nyingine

## 4:2 Kuathiriwa kwa mwandishi na mazingira mbalimbali: udhanaishi

Kwa maelezo ya *Encyclopedia Americana* (1929 762) udhanaishi umeelezewa kama:

> Ambao huhusisha mitindo na imani mbalimbali. Hata hivyo, moja ya sifa yake muhimu, ambayo imeelezewa na asili ya ulimwengu, ni kujishughulisha kwake na kuwepo kwa binadamu Hususan, hukubali uhuru wa binadamu na kukataa dhana zenye misingi ya kijamii inayodunisha kuwepo kwa binadamu. Huwasilisha maasi dhidi ya mawazo na asasi ambazo huzuia uhuru wa binadamu na kupinga uwajibikaji.
>
> (Tafsiri yetu).

Hii ina maana kwamba binadamu anaweza kuyaendesha maisha yake atakavyo na kuwa ana uhuru wa kuamua atakavyo yeye. Kwa muktadha huu basi matendo ya binadamu, hata yawe mabaya, yamo katika uwezo wake wa kuamua kutenda baya au zuri.

Kamusi ya Fasihi ya Cassell (1953:213) nayo imefasili udhanaishi na kusema kwamba:

> Kuna makundi kadhaa ya kifalsafa ambayo yapo chini ya udhanaishi na yote hutilia mkazo uhai wa binadamu na udhabiti wa tajriba yake kinyume na nadharia zisizo na mashiko za kuwazika tu
>
> (Tafsiri yetu)

Fasili hii nayo basi imetilia mkazo hoja ya kuwepo na uhai wa binadamu Tajriba na matendo ya binadamu yana udhabiti na yanaweza kuonekana Itakumbukwa ni katika kipindi hiki cha kuzuka kwa mwelekeo huu (wa kidhanaishi) ambapo kulikuwa na mwelekeo mwingine uliopinga kuwepo (uhai) kwa binadamu na kudai kuwa binadamu hawezi kutetea dai la uhai wake. Falsafa hii basi ilizuka ili kupinga falsafa zilizokuwa na mwelekeo wa aina hii

Kwa muktadha huu basi kazi hizi mbili za Kezilahabi (*Nagona* na *Mzingile*) ni kazi ambazo zimeandikwa kuegemea falsafa ya kidhanaishi Kama vile ambavyo tumekwisha jadili katika sura ya pili na ya tatu mwandishi huyu ameandika kwa kirefu juu ya maisha ya binadamu Kazi yo yote yenye kuelezea maisha na kuwepo kwa binadamu huwa imeegemea mkondo wa falsafa ya udhanaishi Kama ambavyo tulikwisha dokeza hapo awali (tazama sura ya kwanza) kichocheo kikubwa kwa mwandishi kuandika kazi hizi mbili kilikuwa kutaka kueleza maisha ya binadamu kama ayaonavyo yeye Kwenye jalada la *Nagona* imeandikwa hivi:

> Nagona ni riwaya inayothibitisha upevu wa falsafa ya Kezilahabi kuhusu dhana ya maisha.

Na kwenye jalada la Mzingile imeandikwa hivi:

> Mzingile ni riwaya pevu inayohusu maisha

Aidha tumekwisha bainisha vile ambavyo mwandishi ameyasawiri maisha ya binadamu kama ambayo yanatawaliwa na vurumai tupu na ni kilinge ambacho hata na yeye mwenyewe (binadamu) hakielewi.

Moja ya sababu muhimu ya Kezilahabi kufuata mwelekeo wa udhanaishi ni athari alizopata maishani (hasa katika shule). Kulingana na M.M. Mulokozi (1983:1), Kezilahabi alizaliwa katika kisiwa cha Ukerewe mwaka 1943. Alielimishwa katika seminari ya Kikatoliki ya Nyegezi, ambako alijifunza falsafa za kidhanifu za dini, lugha ya Kilatini na masomo mengine ya kawaida. Baada ya kidato cha VI alifukuzwa katika seminari kwa sababu walimu wake walisema hakuwa na 'wito' wa kutosha kwa kazi ya upadre.

Nadharia ya kisosholojia hutilia mkazo mazingira yaliyoizaa kazi ya kifasihi. Mwandishi anaelekea kuamini kuwa hali ya nchi yake ya Tanzania ilikuwa ya kukatisha moyo kutokana na matatizo mengi

yaliyokithiri sawa na ya kipindi cha mwanzo mwanzo wa miaka ya 40 ambapo falsafa ya udhanaishi ilipata nguvu huko Ulaya. Hususan mwegemeo ambao ulitawaliwa na imani ya kutokuwepo kwa Mungu. Hata hivyo hali hizi haziwezi zikamithilishwa moja kwa moja kutokana na tofauti za kihistoria. Aidha hali siyo (na haikuwa) mbaya huko Tanzania sawa na ilivyokuwa huko Ulaya na Kezilahabi amehukumiwa na wahakiki wengi kwa kuchukua mwelekeo huu wa uandishi.

Hiki kilikuwa ni kipindi cha vita vikuu vya pili (1939-1945). Katika vita hivyo kulikuwa na uharibifu mkubwa wa mali na uhai. Watu wengi walipoteza maisha yao ilhali wengine waliachwa wakiwa viwete huku wengine wakiathiriwa kwa jinsi mbalimbali na zana za kivita zilizotumika. Jamii zilivurugwa na mila na desturi zikavunjika huku jamaa wa jamii moja wakitawanywa ovyo. Ni katika hali kama hii ambapo falsafa hii ilishika nguvu. Maisha ya binadamu yalianza kuelezewa kama ambayo hayana maana yoyote. Hii ilifuatia kushuhudiwa kwa watu maelfu kwa maelfu wakifa kufuatia vita hivi - na basi wanafalsafa wakajiuliza maana ya kuishi ni nini?

Waaidha mataifa haya ya magharibi yalikuwa yamepiga hatua kubwa za kimaendeleo. Viwanda vya kutengeneza bidhaa mbalimbali vilikuwa vimechipuka na uvumbuzi wa binadamu ulikuwa umemwezesha kupiga hatua katika kujiendeleza. Vita vilipozuka mambo haya yote yalivurugwa na viwanda vingi vikaharibiwa. Maisha ya binadamu basi yalionekana

hayana maana kwani maendeleo makubwa ambayo alikwisha yapata yalikuwa si kitu tena, si chochote. Mwanafalsafa na mwandishi mashuhuri wa tapo mojawapo la udhanaishi, Albert Camus (1913-1960) aliwahi kushiriki katika vita hivi na alijiunga na upande wa Ufaransa. Msimamo wake na utetezi wa madai yake basi bila shaka uliathiriwa kwa jinsi kubwa na vita hivi (tutajadili kuathiriwa kwa mwandishi na waandishi wengine katika sehemu inayofuata). Imani yake ya maisha ya binadamu kutokuwa na maana ilikita mizizi.

Ingawa hali hii ni tofauti na mazingira ambayo Kezilahabi ameandikia,kutofaulu kwa nchi yake na kuwepo kwa matatizo mbalimbali kumempelekea kuwa na mwelekeo wa kidhanaishi. Matatizo haya yanaanza tangu wakoloni walipokuja nchini Tanzania na kuwafanya Waafrika watumwa wao. Chini ya utawala wa mkoloni Mwafrika alinyanyaswa na kunyimwa haki. Maisha ya Waafrika yalitawaliwa na umaskini na unyonge. Kutokana na kunyimwa haki zao na kudhalilishwa kwa Waafrika, wao walichukua zana na kuanza kupigania uhuru. Watu wengi walikufa na vilevile mali zisizo kiasi zikaharibiwa. Ingawa uharibifu wa mali na maafa haya hayawezi kufananishwa moja kwa moja na hali ilivyokuwa huko Magharibi, Kezilahabi amechukua mwelekeo wa udhanaishi kutokana na kuathiriwa kwake na matukio haya ya kihistoria.

Baada ya kujipatia uhuru Waafrika walikuwa na matumaini makubwa kuwa watapata haki zao, umaskini utakwisha na hawatadhalilishwa tena na serikali ya Mwafrika mwenzao. Lakini hali haikubadilika, umaskini

ulikithiri, wanyonge hawakuwa na haki tena na ilikuwa kana kwamba serikali ya Mwafrika ilikuwa ni ya mkoloni mweusi. Katika *Nagona* tunaona sheria ikizuiliwa kuchukua mkondo wake kutokana na ulaji rushwa na wenye pesa ambao wako tayari kuzuia haki isitekelezwe. Padre na msimulizi wanajibizana hivi:

> "Ulitoa msaada wowote kuzuia ushahidi au haki isitendeke?"
>
> "ndiyo."
>
> "Kwa mfano?"
>
> "Niliwapa pesa mahakimu." (uk. 49)

Hapa mwandishi anaonyesha kuwa wanyonge hawana haki kwani haki yao imechukuliwa na wenye pesa. Wenye pesa wanavunja sheria kwa kuua (kwa kuwapa watu pesa wafanye hivyo) lakini hata mtuhumiwa mkuu hafikishwi mahakamani. Wale ambao wanafikishwa kortini ni waliopokea pesa (uk. 48). Na ni ajabu kwamba ni mtuhumiwa mkuu ndiye anayezuia haki isitekelezwe.

Matatizo haya, kama yale ya Magharibi wakati wa vita vikuu vya pili, ndio yaliyompelekea Kezilahabi kujiuliza je ni nini maana ya maisha? Mwandishi ameiona serikali ya Tanzania kama ambayo imefeli katika majukumu yake. Baada ya mkoloni kuondoka na nchi hii kujipatia uhuru, baadaye ilikumbatia siasa za ujamaa katika maongozi yake. Mwandishi

ameukosoa vikali mfumo huu wa uongozi katika riwaya zake zingine, hasa *Gamba la Nyoka* Itakumbukwa vilevile kuwa siasa na chumi za nchi huenda sambamba Siasa za ujamaa zilitetea uzalishaji mali wa pamoja. Ilibidi watu wahamishwe makwao ili waweze kuishi katika vijiji vya ujamaa ambapo wangefanya kazi kwa pamoja. Mwandishi anaiona njia hii ya uchumi kama iliyochakaa ndipo msimulizi akasema katika *Mzingile:*

> .... chama kikawa na kauli ya mwisho juu ya kila kitu Kikashika hatamu. Kikawaongoza watu kwenye vichochoro vya uchumi vilivyoachwa kutumika zamani... (uk 44).

Mwandishi hapa anaiona siasa ya ujamaa kama ambayo ilichukua mwongozo ambao haufai Itakumbukwa vilevile kuwa chama cha serikali inayotawala ndicho ambacho hutoa maongozi na sera za serikali Chama Cha Mapinduzi (C.C.M) kiliamua kufuata sera za ujamaa katika Azimio la Arusha la mwaka wa 1967. Moja ya tetezi muhimu ya siasa za ujamaa kama ambavyo huelezewa na nadharia ya Marx ni usawa wa binadamu na kuondoa tofauti za kiuchumi baina ya watu - yaani kuondoa matabaka Mwandishi anawaita wanasiasa hawa walevi kwani wanayoyaimba hawatekelezi na siasa zao ni potovu (Mzingile). Mzee na msimulizi wanajibizana hivi:

"Wanasema watagawana wenyewe sawa kwa sawa na kuondoa matabaka."

"Matabaka! Mbona mnatunga maneno ambayo hayamo katika kamusi yangu!" (uk. 15).

Hapa mwandishi anaelekea kumaanisha kuwa usawa, kama ambao hutetewa na siasa za ujamaa, hauwezi ukafikiwa. Kama ambavyo tumekwishadokeza hapo juu siasa za ujamaa zilihitaji kutaifishwa kwa mali, kuchuma na kuzalisha mali kwa pamoja. Wale ambao walikuwa na mali yao ingetwaliwa na watu wote wangekuwa sawa. Hii ingekuwa ni katika kuhakikisha kuwa hakuna matabaka ya wenye mali na maskini (wanyonge) - wasio na mali. Mwandishi alishuhudia mazingira haya ya kisiasa, na yakaathiri utunzi wake, athari ambazo tunazishuhudia katika kazi zake. Hata hivyo serikali ya sasa ya Tanzania imewachilia mbali siasa hizo na hufuata siasa za kibepari (Senkoro 1995:67).

Ni kutokana na matatizo mengi ya nchi yake na nchi za ulimwengu wa tatu kwa jumla ndipo mwandishi akaisawiri dunia kama mahala pa fujo, vurumai na vurugu. Matatizo hayo ni pamoja na ongezeko la gharama ya maisha, ufisadi na wizi wa mali ya umma hali ambayo hupelekea kukosekana kwa huduma bora za afya na kuwania vyeo katika chama na serikali (*Mzingile* uk. 45). Itakumbukwa kwamba haya ndiyo matatizo sugu ambayo yanazikabili nchi changa za Afrika. Hasa nchi ya Tanzania ni baadhi ya nchi zenye umasikini mkubwa ulimwenguni na mazingira ya

aina hii yaliathiri uandishi wa Kezilahabi katika kutunga kazi hizi mbili Alishuhudia kuteseka katika umaskini kwa jamii alimoandikia.

Matatizo haya hayaikumbi nchi ya Tanzania tu bali nchi nyingi za ulimwengu wa tatu, kama ambavyo msanii huyu ameandika Nchi ya Tanzania imetumika tu kama mandhari kwani masuala ambayo yameongelewa siyo ya Tanzania pekee bali ya jamii pana ya mataifa ya ulimwengu wa tatu na ulimwengu kwa jumla. Kezilahabi kama mwandishi anayeishi katika ulimwengu wa tatu ameyashuhudia na hata kusikia visa mbalimbali vinavyotendeka katika ulimwengu huu. Katika *Nagona* msimulizi anasema

> Nchi yetu ilikuwa imekumbwa na janga la njaa Nchi nyingi katika ulimwengu wa watu zilipata pigo kubwa na mamilioni ya watu walikufa Migogoro mingi ya kiuchumi iliendelea kuisakama dunia (uk. 18).

Nchi nyingi za ulimwengu wa tatu (hasa nchi za Afrika) hukabiliwa na janga la njaa, vita vya wenyewe kwa wenyewe na migogoro ya kiuchumi Aidha viwanda vingi vyenye kusimamiwa na serikali hufanya kazi kwa hasara hasa kutokana na usimamizi mbaya

Mwandishi kama ambaye anaishi kati ya jamii pana ya ulimwengu wa tatu ameathiriwa na jamii hiyo. Ni kutokana na mazingira hayo ambayo

ameweza kujitokeza na suala la maana ya maisha ambalo halihusu ulimwengu wa tatu pekee bali binadamu kwa jumla na maisha yake ulimwenguni.

Matatizo haya yamechangia katika kupelekea mwandishi kuamini kwamba duniani hakuna furaha na maisha ya binadamu yametawaliwa na vurumai tupu. Kezilahabi anaona kwamba fujo na vurumai ndizo zitakazoleta maana halisi ya maisha. Ni suluhisho hili ambalo limempelekea Senkoro F.E.M.K (1995:61) kuuliza:

> Labda inatubidi tujiulize sisi wasomaji, ni kwa nini waandishi wengi wa fasihi ya Kiswahili ya Tanzania ya miaka 80 na 90 walitoa jawabu hili la fujo, vurumai, vurugu na matumizi ya nguvu kuwa ndilo litakalotutoa katika majanga waliyoyaongelea katika kazi zao za fasihi.

Lakini matatizo na maafa ambayo mwandishi ameyaongelea hayaishi na yanaendelea kuisakama nchi yake na nchi zingine za ulimwengu. Kezilahabi ameyashuhudia matatizo haya yakiendelea na kuendelea bila kikomo hali ambazo zimempelekea kuipaka dunia rangi ya fujo, vurugu na vurumai tupu. Waaidha siyo mahali ambapo binadamu atawahi kuipata furaha. Maoni haya ni sawa na ya Albert Camus aliyedai kuwa binadamu hujaribu kuishi katika ulimwengu bwege (absurd). Mawazo yake tutayatazama kwa upana zaidi katika sehemu inayofuata

### 4:3 Athari nyinginezo

Mwandishi huyu ameathiriwa na kazi za waandishi mbalimbali wenye mwelekeo wa kidhanaishi. Yeye aliwahi kukiri [5]kuathiriwa kwake na mwandishi mashuhuri, Albert Camus (1913-600). Yeye (Camus) aliamini kuwa mahali pa binadamu ulimwenguni ni duni katika ulimwengu duni (1977:762). Wahusika wengi katika vitabu vyake wanaamini binadamu hana maana yoyote. Maoni haya yanaoana na ya Kezilahabi anaposema kuwa ulimwengu tambara bovu (*Nagona* uk. 24). Sitiari hii inayoonyesha kuwa dunia ni mahali pabaya na pasipofaa kwa maisha ya binadamu. Katika kazi zake mbili Kezilahabi ametusawiria dunia kama mahali pa vurugu na vurumai. Kezilahabi kama Camus anayaona maisha ya binadamu hayana maana yoyote kwani anasema ujasiri wa mja hukamilishwa na kifo. Na maisha yenyewe ni mzaha mtupu na ndio maana yanaweza kuishika (*Mzingile* uk 13-14).

Maoni haya vilevile yanaoana na ya Samuel Beckett ambaye alikuwa mwandishi wa riwaya na tamthilia pia. Kwa madai ya Beckett (1975:256) binadamu ni kiumbe aliyetengwa na kuwekwa katika ulimwengu wenye masuala mengi yasiyopendeza. Nyingi ya kazi zake ambazo zilionyesha dunia kama mahala pa mateso, ziliigizwa katika kile ambacho kilikuja kujulikana kama drama ya ubwege (Theatre of the absurd). Katika nyingi

ya kazi zake dunia imeonyeshwa kama mahala pa mateso mengi na maafa kama ambavyo tumeyashuhudia na kujadili katika *Nagona* na *Mzingile.*Riwaya ya Beckett, *How it is*, inaonyesha maisha ambayo yametawaliwa na mandhari ya ajabu ajabu kati ya giza na matope. Hali hizi tumezimithilisha na bonde, maluweluwe na sehemu za ajabu ajabu katika *Nagona* na *Mzingile* ambazo wahusika wa Kezilahabi wanajikuta.

Maoni ya Kezilahabi kuwa ukweli hauwezi ukapatikana katika ulimwengu yameoana moja kwa moja na ya Soren Kierkegaard (1813-55) aliyedai kuwa ukweli wenye umuhimu hauwezi ukapatikana moja kwa moja (1977:762). Alisema kuwa ukweli hutegemea mtu - kwamba ukweli ni ukweli tu katika miktadha ya watu mbalimbali. Motifu ya kusaka ukweli imetawala katika *Nagona*. Ukweli huu unawakilishwa na paa ambaye tangu mwanzo msimulizi amekuwa akifuatilia nyayo zake. Anapofanikiwa kumpata anamponyoka kutokana na utelezi wake. Kama ambavyo tumejadili suala hili kwa kirefu katika sura ya tatu binadamu hataweza kuupata ukweli kwani anasema "....usijidai kuwa na ukweli mikononi mwako." (*Nagona* uk. 43). Katika Mzingile vile vile msimulizi yumo mbioni kutafuta ukweli ambao haupatikani

Kierkegaard sawa na Friedrich Nietzsche walitilia mkazo hoja ya binadamu kufikiri Hasa Friedrich Nietzsche alidai kuwa ubunifu wa binadamu utamwondoa katika genge la watu duni (1975:1941). Ubunifu wa binadamu kwa upande mwingine utafanikiwa tu kutokana na binadamu

kufikiri. Haja ya binadamu kufikiri imekaririwa ukurasa hadi ukurasa katika kazi hizi mbili za Kezilahabi. Katika *Nagona* babu anasema hivi:

> Usiwe na haraka kuna vikwazo vingi, lakini kushinda vikwazo si kuifikia kweli. Safari ni ndefu, lakini kusafiri si kufika . Jambo muhimu ni <u>kufikiri.</u> (uk. 24)
> (msisitizo wetu)

Babu anamwusia msimuluzi asiwe na haraka au papara katika kuusaka ukweli. Ili kuweza kuupata ukweli kuna vikwazo vingi (tazama sura ya tatu). Lakini mwandishi anatahadharisha kuwa kushinda vikwazo hivi siyo kuufikia ukweli kwani 'kusafiri siyo kufika ' Hata hivyo jambo muhimu na ambalo anasisitiza ni kufikiri na kuwaza ili kukaribia ukweli ambao haupatikani kirahisi.

Katika *Mzingile* (uk.50-52) hoja ya binadamu kufikiri ili kuweza kujivumbulia maendeleo mapya imekaririwa. Mwandishi amemsawiri binadamu akiwa katika ghera ya kufanya majaribio katika viwanda na maabara ili kuweza kujiondolea baadhi ya madhara yanaoletwa na ubunifu wa binadamu. Ubunifu huu ndio Nietzsche aliosisitiza aliposema kuwa ubunifu wa binadamu utamwondoa katika genge la watu duni.

Kufikiri kwa maana huanza katika kujielewa mwenyewe mwanzo walidai wote Kierkegaard, Nietzsche na Karl Jaspers (1977:762). Katika *Nagona* na *Mzingile* vilevile tumeona binadamu akifanya juhudi kubwa za

kujielewa mwenyewe Katika *Nagona* tunashuhudia binadamu akiwa katika mjadala mkubwa na nafsi yake juu ya roho na mwili wake (uk 39-40). Hii ni katika ghera ya kujifahamu nafsi yake kabla hajafahamu ulimwengu wake. Katika *Mzingile* binadamu anaanza kufikiri kwa kuwaza juu ya uhai wake kabla ya kufanya majaribio ya uvumbuzi wa ulimwengu wake (uk.50-51). K.W Wamitila (1997 16) amedai kuwa Socrates, ambaye huenda alikuwa mdhanaishi wa kwanza aliwaasa wanafalsafa wajijue wenyewe kwanza, " know thyself". Msingi wa imani ya Kezilahabi basi umejikita katika kazi za wanafalsafa hawa mashuhuri wa udhanaishi.

Aidha mwandishi huyu ameathiriwa vilevile na kazi za Martin Heidegger. Katika *Nagona* tumeona vile ambavyo binadamu hana hiari na matukio maishani mwake na mara kwa mara yanakuwa kama ajali. Athari na imani hii inatokana na madai ya Heidegger kuwa binadamu anashurutishwa kuitegemea ajali, wazo ambalo hujaribu kulitoa mawazoni mwake, lakini hawezi kuikwepa hali hii kwa vyovyote vile (1975:1216). Kama ambavyo tumedai katika sura ya tatu motifu ya ajali imetumika kutudhihirishia kuwa binadamu hana cho chote ambacho anaweza kujipangia. Matukio yote maishani mwake ni ajali tu. K.W Wamitila (1997:16) amesema kuwa katika mazungumzo yake na mwandishi huyu, alikiri kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na waandishi wa udhanaishi, Martin Heidegger na Friedrich Nietzsche.

Suala lingine ambalo limejitokeza katika kazi hizi na kazi nyinginezo za Kezilahabi na ambalo tunaweza kuona asili yake katika udhanaishi ni kupuuza kwake kwa dini Katika sura ya II tumelijadili suala hili kwa kirefu na mwenyewe Kezilahabi amekariri msimamo wake katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1977:59) kupitia mhusika Rosa anayesema

> Wokovu maana yake ni nini? Wokovu! Wokovu gani! Kama kuna moto basi nitakwenda

Hapa mwandishi anapingana na imani ya kumtegemea Mungu na wokovu ili kuweza kumtatulia matatizo yake Katika *Nagona* vilevile tumeona Babu akidai kuwa padiri anachezea ngoma yake nje ya duara (uk 10) kumaanisha kuwa imani katika dini haitamtatulia binadamu shida zake wala haitampa jawabu la ukweli anaousaka. Aidha hii ni moja ya athari alizopata katika maisha yake ya kiseminari Msimamo wake kuhusu dini unadhihirisha uasi wa maisha ya kuandaliwa kuwa padre

Maoni haya tunayamithilisha na ya Jean-Paul Sartre ambaye alidai kuwa hakuna Mungu na hivyo basi hakuna silika imara ambayo humshurutisha binadamu kutenda jambo fulani (1975:2427) Anamtizama binadamu kama mwenyewe kuwajibika kwa matendo yake lakini mwenye upweke katika uhuru unaoogofya wa kuchagua na kujiendeleza katika ulimwengu usiokuwa na maana. Sartre vilevile alikuwa mwanajeshi katika vita vikuu vya pili. Aliamini kuwa binadamu atajiletea maadili na uadilifu maishani

mwake wala siyo kwa kutegemea Mungu Pengine aliyeiwekea nukta hoja hii ni Friedrich Nietzsche katika madai yake kuwa kanisa ni kaburi la Mungu (1977:762) Kezilahabi ameathiriwa vikubwa na hoja hizi ambazo zimejitokeza katika kazi zake

Mtazamo wa mwandishi wa maisha unaweza kuwa uliathiriwa na maisha yake ya shule Waaidha maisha yake ya shuleni yanaweza kuwa kwa kiasi kikubwa yaliathiri mtazamo wake wa suala la Mungu. Kezilahabi alikuwa amejiunga na seminari kwa muda wa mwaka mmoja ambako alianza masomo yake ya dini. F.E.M.K Senkoro (1995:62) anasema kuwa mahali hapa panaonyesha athari kubwa katika kazi zake za fasihi Hata hivyo hakuwahi kukamilisha masomo haya na akafukuzwa shuleni humo kutokana na kile kilichoitwa na walimu wake kutokuwa na 'wito' wa kutosha. Ni kumbumbu hii inayomjia katika *Mzingile* kupitia msimulizi ambaye anasema:

> mimi nilikuwa nikilia tulipotoka kanisani rafiki zangu walinipa pole kwa kushindwa mtihani Walinisaidia kufunga mizigo Nilipokuwa naondoka Padiri mmoja alikuwa nyuma yangu akinifukuza kama mbwa "Nenda nyumbani kwa mama yako! Wewe hukuteuliwa! Wewe ni mwizi tu wa ujuzi!".....(uk.23)

Nadharia ya kisosholojia hutilia maanani maisha ya mwandishi - kufaulu, kutofaulu na matamanio yake maishani. Kwa muktadha huu tunaona Kezilahabi akishindwa kufaulu katika mtihani wa dini. Matokeo yake yalikuwa kupuuza dini na kuwa na mwelekeo wenye kupinga kuwepo kwa Mungu.

Aidha katika kazi zote mbili za Kezilahabi tumeona matumizi makubwa ya maneno ya Kilatini. Hii ndio lugha ambayo hutumika katika kutoa maagizo mengi ya dhehebu la kikatoliki na ni lugha aliyojifunza katika seminari. Vilevile amewataja wanafalsafa mashuhuri ambao wengi wao tumeona jinsi walivyoathiri mtazamo wake wa masuala ambayo yamejitokeza katika kazi zake. Amewataja: Plato, Socrates, Aristotle, Hegel, Freud, Darwin na Nietzsche (*Nagona* uk.15).

Hata hivyo kile ambacho watu wengi wanachukia wanaposoma kazi nyingi za Kezilahabi ni jinsi anavyoyajadili na kuyagubika giza masuala ya maisha, kifo, ukweli,furaha, Mungu na uasi wa dini. Wahakiki wengi vilevile hawaonekani kuvutiwa na falsafa ambayo Kezilahabi anayoendeleza ambayo inamwonyesha binadamu kama kiumbe aliyeumbiwa mateso.

Ingawaje tunaweza kuelezea kuegemea kwa mwandishi katika udhanaishi kwa mtazamo wa kuanguka kwa siasa za ujamaa nchini Tanzania na matatizo mbalimbali ya nchi changa za Afrika, swali ambalo tunajiuliza ni,

je, mazingira na hali ni mbaya sawa na ilivyokuwa katika mazingira ambamo udhanaishi ulipata msisimko mpya huko Ulaya? Kama ambavyo tumeeleza hapo awali mtazamo wa udhanaishi ulipata nguvu na wafuasi wengi kutokana na hali halisi za kihistoria. Ni mwelekeo ambao ulikuwa na mtazamo wa kukata tamaa na imani mbalimbali. Hiki kilikuwa ni kipindi cha vita vikuu vya pili

Aidha tumethibitisha kuwa baadhi ya waliokuwa watetezi wakuu wa mwelekeo huu walikuwa wanajeshi na walishiriki katika vita hivi. Kwa wakati huu suala muhimu ilikuwa kujishughulisha na uhai na watu wengi walijitambulisha na kufanya bidii katika kuelezea dhana za maisha, furaha, woga na Mungu. Baadhi yao walishuhudia uharibifu mkubwa na maafa yaliyoletwa na vita hivi.

Hata hivyo hoja muhimu ilikuwa kuweza kubainisha jinsi Kezilahabi alivyoathiriwa na udhanaishi. Tumejaribu kuonyesha chembechembe za falsafa ya udhanaishi ambazo zimejitokeza katika kazi hizi mbili pamoja na kuoanisha hali hizo na matukio na hali halisi za kihistoria kama ambavyo nadharia tunayotumia inavyoturuhusu.
Aidha tumeona jinsi mwandishi alivyoathiriwa na watetezi na kazi mbalimbali za udhanaishi

## 4:4 Hitimisho

Katika sura hii tumechunguza ni katika mazingira yapi ambamo kazi hizi mbili ziliibuka Katika mazingira ya kisiasa tumeona mwandishi akizikosoa siasa za mataifa ya ulimwengu wa tatu ambazo zimetawaliwa na ufisadi, wizi wa mali ya umma, kiburi, uonevu, ubinafsi, ubarakala na mauaji ya kisiasa Mwandishi aliyashuhudia baadhi ya mambo haya yakitendeka katika nchi yake changa, Tanzania huru Aidha mataifa haya tumeona jinsi ambavyo hayana uwezo dhidi ya siasa za mataifa yenye uwezo mkubwa na yenye zana hatari za kivita kama mabomu ya nyuklia

Hali ya kiuchumi vilevile ni ya kuvunja moyo. Nchi ya Tanzania, kama nchi nyingi za ulimwengu wa tatu, imo katika matatizo makubwa ya kiuchumi. Mwandishi anaona kuwa hizi ndizo hali zinazotawala mataifa haya yaani viwanda vingi vimekufa ilhali vingine vinafanya kazi kwa hasara (*Nagona* uk 18). Maongozi ya kiuchumi nayo ni ya kusikitisha kwani kama Kezilahabi asemavyo chama kiliwaongoza watu kwenye vichochoro vya uchumi vilivyoachwa kutumika zamani (*Mzingile* uk. 44) Ni kutokana na siasa basi tunapata uchumi ukisambaratika kushuka kwa thamani ya pesa, mpumko wa bei za bidhaa, ufisadi na wizi wa mali ya umma. Kama ambavyo tumesema, nchi ya Tanzania ni kati ya mataifa maskini sana duniani. Bila shaka mazingira ya kiuchumi ya aina hii yaliathiri mwandishi vikubwa

Kutokana na hali hizi jamii ya Tanzania ndio iliyokereka zaidi na mwandishi akashuhudia hali hii. Watu wengi wanasakamwa na njaa, maafa mengi yanatokea na basi akajiuliza , maana ya maisha ni nini? Matatizo haya yanapelekea binadamu kukosa sifa muhimu za utu ambazo ni wema, imani, na upendo Badala yake miongoni mwa jamii panakuwa na uwingi wa uchoyo, kiburi, uonevu, na ubinafsi (*Mzingile* uk 5)

Ni hali na mazingira haya ambayo yanampelekea mwandishi kuwa na mwelekeo wa kidhanaishi Katika sura hii tumechunguza hali zilizofanya udhanaishi kupata nguvu mpya huko magharibi na jinsi mwandishi alivyoathiriwa na kazi mbalimbali za waandishi wa udhanaishi

**TANBIHI**

[1] Robert, Shaaban (1954) Kielezo cha Insha. Witwatesrand university press, Johannesburg, uk 1

# 5:0 SURA YA TANO

## HITIMISHO

### 5:1 Muhtasari wa masuala muhimu

Katika tasnifu hii tumeshughulikia kazi mbili za Euphrase Kazilahabi ambazo ni *Nagona* na *Mzingile* Ni katika kazi hizi mbili ambapo falsafa ya mwandishi kuhusu maisha imejiweka bayana zaidi Aidha tumejadili jinsi msimamo na mtazamo wake wa maisha umeathiriwa na mazingira mbalimbali pamoja na maisha yake mwenyewe

Katika sura ya pili tumezitalii juhudi mbalimbali za binadamu za kusaka ukweli unaodhihirishwa na maisha yake Lakini katika juhudi hizi inakuwa kama kwamba anazunguka kwenye duara huku akirudi alikoanzia Juhudi za binadamu zinaemewa na mwandishi anatoa rai kwa kutumia motifu ya kufikiri. Aidha juhudi hizi zinapata changamoto katika ari ya binadamu kujiimarisha kiviwanda

Waaidha tumeona jinsi binadamu amekimbilia sehemu mbalimbali katika sakasaka zake za ukweli unaodhihirishwa na maisha yake Mashujaa waliowahi kuishi hawampi jibu - badala yake walifaulu tu katika kuiwekea njia daraja ambazo hazivukiki Asasi mbalimbali za binadamu pia hazimpi jibu Mwanzo ni dini ambayo kama asasi muhimu imeshindwa katika majukumu yake. Viongozi wake wameonyeshwa wakiwa wamekufa

moyo na kusalimu amri kwa kujiingiza katika anasa Pili ni serikali ambayo imeongeza kilinge katika kitendawili cha maisha kwa kusababisha maafa, vurugu, na kuzorota kwa uchumi Hatimaye elimu ya binadamu inakuwa hatari hata kwa maisha yake yenyewe ilhali alidhani itamtanzulia tanzu

Katika sura ya tatu tumejadili maana ya maisha kama ambavyo imejibainisha katika kazi hizi Kama ambavyo anwani ya moja ya novela hizi inavyoelekeza, kulingana na mwandishi maisha ni mzingile, Ni mzingile mwanambije wenye mizingo isioelekeza kwenye mlango wa kutokea Na kama ambavyo tumenukuu kutoka kazi zake zingine, Kezilahabi ameyaweka mawazo yake wazi kuwa maisha ya binadamu ndiyo adhabu kali aliowahi kupatiwa - kuyatunza. Ni kama ambayo yanamkejeli kwani , amelemewa na kupata uhalisi wake Aidha tumeonyesha kuwa kwa Kezilahabi maisha ni vurugu tupu

Ingawa mtazamo huu wa mwandishi umeathiriwa na mazingira na waandishi mbalimbali huku ukiegemea falsafa ya udhanaishi, Mbatiah (1996 :16) amesema kuwa hali ambazo zilipelekea mtazamo wa aina hii huko Magharibi ( ambao mwandishi amefuata ) zilikuwa ni kutokana na vita vikuu vya pili Amedai kuwa waandishi wenye kufuata mwegemeo wa falsafa ya udhanaishi waliafikiana na mazingira ya kijamii ya wakati huo. Licha ya ukweli katika kauli hii, tumetaja kwamba mwandishi ameathiriwa vikubwa na hali na matatizo sugu ya ulimwengu wa tatu (ambako

anatoka) na kuyamithilisha mazingira hayo na yale ya kipindi udhanaishi ulipopata mwamko mpya huko Magharibi

Aidha tumeyajadili masiala ya furaha na ukweli katika sura hii. Tumeona taswira aliyotuchorea msanii huyu ya maisha ya binadamu yakiwa yametawaliwa na maafa mbalimbali Toni ya huzuni imeshamiri katika kazi hizi mbili kutokana na maafa mbalimbali ambayo yamestawi na ambayo yanasababishwa na ajali mbalimbali. Viongozi nao wanavuruga amani na dunia inakuwa mahala pa fujo na vurugu Sifa muhimu zinazoushikilia mhimili wa binadamu, ambazo ni wema, imani na upendo zinazokosekana, na basi mhimili huu ni kana kwamba unaelekea kuporomoka (*Mzingile* uk.5).

Ukweli nao umemkwepa binadamu kokote kule anakousaka. Ukweli, ambao unawakilishwa na sitiari ya mwanga, ni muhali kuutia mkononi. Kama mwanga ulivyo -ndivyo ukweli ulivyo - hauwezi ukashikika. Aidha una sifa ya utelelezi na kutodhibitikika

Hatimaye katika sura ya nne tumetizama jinsi mwandishi huyu ameathiriwa na mazingira ya kihistoria na ya kijamii katika kazi zake. Mwandishi ameubeza mfumo wa uchumi wa kisoshalisti na kuuona kama uliochakaa na kuachwa nyuma na wakati. Mfumo huu ulitimika nchini Tanzania baada ya Azimio la Arusha la mwaka wa 1967 hadi miaka ya 90.

Tumeona jamii za ulimwengu wa tatu zikiwa katika matatizo makubwa ya kisiasa na kiuchumi na ni kama kwamba mwandishi anaelekea kuuliza maana ya maisha basi ni nini?

Tumeona jinsi mwandishi huyu ameegemea sana katika falsafa ya udhanaishi katika utunzi wake. Hali hii imepelekewa na athari alizopata kutoka kwa waandishi wa fasihi ya uduni na mazingira alimoandikia, kama ambavyo tumedai. Aidha kama ambavyo Senkoro (1995:62) amedai, maisha yake katika seminari yaliathiri mtazamo wake vikubwa mno na chembechembe za athari hizo zimejitokeza katika kazi hizi mbili

Kuhusu mwegemeo huu Mbatiah (1997: 16) amedai kuwa fasihi ya aina hii haielekei kuwa na umuhimu mkubwa katika mazingira ya Afrika Mashariki. Naye Wamitila (1997:23) ametoa kauli kuwa wahakiki wanaweza kumlaumu Kezilahabi kwa kuua riwaya ya Kiswahili ikiwa bado katika uwanagenzi. Mbali na ukweli katika kauli hizi, kupitia kazi za *Mzingile* na *Nagona* mwandishi huyu ameinua kiwango cha fasihi ya Kiswahili na kufikia mawanda mapana hata zaidi. Uwezo wake wa kufinyanga lugha na kuibuka na sanaa ya namna yake ni hatua katika kukuza na kupanua fasihi ya Kiswahili.

## 5:2 Mapendekezo

Katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya kisosholojia ili kutuwezesha kusaili ni jinsi gani mazingira mbalimbali na kazi za waandishi wengine zimeathiri utunzi wa kazi za *Nagona* na *Mzingile.* Tunatoa rai kwa wahakiki kutumia nadharia ya uchanganuzi nafsi (Psychoanalysis). Nadharia hii hutetea dai kuwa mazingira msanii anamoinukia ni muhimu katika mtazamo wake kama ambavyo nadharia ya kisosholojia hutetea. Lakini mojawapo ya kanuni zake muhimu ni kuwa matukio yaliyompitikia binadamu katika uchanga wake hubanwa katika akili yake kisha yakaja kujitokeza baadaye anapokuwa na umri mkubwa. Wamtilia (1997:22) amedai kuwa kuna uwezekano kwamba majaribu ambayo ubongo hupitia huku ukiwa katika safari ya kukomaa ni sawa na mashaka yanayopitikia wasimulizi katika novela hizi mbili. Ametoa kauli kuwa mengi ya yale mwandishi ameyasema katika novela zote mbili ni mawazo ambayo yalibanwa katika akili yake na sasa yamejitokeza.

Kutokana na mipaka na muda uliokuwepo wa kuandika tasnifu hii tumejibana zaidi katika maudhui na kuzungumzia kwa muhtasari sana juu ya fani. Aidha tumetaja katika sura ya kwanza kuwa novela hizi mbili zimedhihirisha kukua kwa mwandishi kiutunzi na kisanaa. Tungependekeza basi wahakiki wazifanyie novela hizi mbili utafiti katika upande

wa fani Kama ambavyo tumedokeza awali msanii ametumia Sitiari, Jazanda na mafumbo mbalimbali katika kuwasilisha ujumbe wake

# MAREJEO


Ansell -Pearson, K (1991) Nietzsche Cotra Rousseau. Cambrige University press. New York

Beckson, E na J Ganz (1960): Literary Terms : A Dictionary. Farrer, Straus and Giroux New York.

Bernander, L (1977) 'Euprase, Kezilahabi - narrator of modern Tanzania'. Lugha. Toleo 1. Jarida la Idara ya Lugha za Asia na za Kiafrika. Chuo Kikuu cha Uppsala Uppsala.

Boesen, J (mhariri) (1977) Ujamaa - Socialism From Above. Scandinavian Institute of African studies. Uppsala

Charlesworth, M (1976) The Existentialists and Jean- Paul Sartre. George Prior Publishers London

Craig, D (mhariri) (1975) Marxists on Literature (An anthology) Penguin Books London

Cruickshank, J (1958) Albert Camus : The Literature of Revolt Oxford University Press. London

Cudon, J A. (1979) A Dictionary of Literacy Terms. Andre Deustch Ltd London

Davis, J C (1963) : Human Nature in Politics : The Dynamics of Political Behaviour John Wiley and sons Inc New York

Encyclopedia American Corporation (1977) : Encyclopedia Americana Grolier Ltd New York

Escarpit, R (1971) Sociology of Literature Frank Cass and company Ltd London

Fischer, E (1959) The Neccesity of Art (A Marxist Approach). Penguin Books London

Freud, S (1961) The Future of an Illusion. W.W. Norton & Co. Ltd New York.

Gachukia, E W (1980) Cultural Conflict in East African Literature. Tasnifu ya Ph.d Chuo Kikuu cha Nairobi Haijachapishwa

Gatare, J K (1993) Dini katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Hall, J (1977) The Sociology of Literature . Longman London

Hussein, E (1971) Mashetani Oxford University Press Nairobi

International Bible Society (1973): Holy Bible. New International Version

Kezilahabi, E (1971) Rosa Mistika Kenya Literature Bureau Nairobi

____________(1974) : Kichwamaji. East African Publishing House Nairobi

____________(1974) : Kichomi. Heinemann Educational Books (E. A) Ltd. Nairobi.

______________( 1981) : Dunia Uwanja wa fujo. Eastern Africa Publications Ltd. Arusha

______________(1988) : Karibu Ndani Dar es salaam University Press. Dar es salaam

______________(1990) : Nagona Dar es salaam University Press Dar es salaam

______________(1991) Mzingile. Dar es salaam University Press. Dar es salaam

Lepp, I. (1968) : Death and its Mysteries Burns and Oates London

Macquarrie, J (1972) : Existentialism World Publishing Co. New York.

Mbatiah, M. (1997) : Mienendo mipya katika Uandishi wa Kezilahabi makala ambayo haijachapishwa.

Mcglashan, A. M. & C.J. Reeve, (1970) : Sigmund Freud Founder of Psycho-analysis Hart-Davis. London.

Michira J. N. (1991) : Kichwamaji : Mgongano wa Tamaduni. Tasnifu ya B.Ed. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa

Mueller, R. W. (1964) : The Testament of Samuel Beckett. Faber and Faber London.

Mulokozi, M.M. (1983) : 'Dunia Uwanja wa Fujo'. Katika Kiswahili . Juzuu 50/1 T.U.K.I. Dar es Salaam

Musau, P M (1985) : Euphrase Kezilahabi: Mwandishi aliyekata tamaa. Tasnifu ya M A Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Ngugi wa Thiong'o (1977) : Homecoming. H.E.B. (EA) Ltd. Nairobi.

Novack, G (mhariri) (1960) : Existentialim versus Marxism : conflicting views on humanism. Dell Publishing Co. Inc., New York.

Nyerere, J K (1967) : Socialism and Rural Development. The Government Printer Dar es salaam

Progoff, I (1955) : Jung's psychology and its social meaning. Grove Press, Inc. New York.

Robert, S. (1954) : Kielezo cha Insha. Witwaterstrand university press. Johannesburg.

Rodney, W (1972) : How Europe Underdeveloped Africa. Tanzania Publishing House. Dar es salaam.

Schur, M.M.D. (1972) : Freud : Living and Dying. International University Press Inc. New York.

Senkoro, F.E.M.K. (1982) : Fasihi. Press and Publicity Centre. Dar es salaam.

_______________(1995) : 'E Kezilahabi : Shaaban Robert wa Pili'. Katika Kioo cha Lugha. Juzuu 1, Na. 1. Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Dar es salaam.

Steinberg, S.H. (mhariri) (1953) : Cassell's Encyclopedia of Literature. Vol. 1. Cassell and Co. Ltd. London.

T.U.K.I. (1981) Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Oxford University Press. Nairobi.

Wambui, B. T. (1992) : Bonde la Wakati Katika Riwaya za Kezilahabi Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Wamitila, K.W. (1991) : 'E. Kezilahabi . A Professor of the Absurd' na ' Nagona and Mizingile : Kezilahabi's metaphysics'. Katika Kiswahili. Juzuu 58 Jarida la chuo cha uchunguzi wa Kiswahili. Dar es salaam.

______________(1997) : 'Contemtus Mundi and Carpe Diem Motifs in Kezilahabi's works. Katika Kiswahili.' Juzuu 60. Jarida la Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili. Dar es salaam.

Warnock, M. (1970) : Existentialism. Oxford University Press. London.

Williams, R. (1974) : Marxism and Literature. Oxford University Press. London.

William, H. Harris & J.S. Levey, (wahariri) (1975) :The New Columbia Encyclopaedia. Columbia University Press. New York.

Wilson, C. (1990) : The Outsider. Victor Gollancz Ltd. London.